**Familia** Prof, Shaba yasimulia ushuhuda baba alivyokata roho



UKURASA 4

**Adaiwa** kuwaua hawara, watoto mgogoro mapenzi

UKURASA 4

**Vijana** wafurahia huduma upasuaji kwa njia ya puto

UKURASA 5



## TEN HAG: MLANGO UPO WAZI SANCHO KUREJEA UTD

UKURASA 21


# Nipashe JUMAPILI

Jumapili Desemba 10, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0581520

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US


# Vipaumbele vinane Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050

UKURASA 2

## Taharuki usiku mnene kuvunjika daraja kati ya Dar, Bagamoyo

UKURASA 2



Mapambano dhidi ya rushwa, ukwepaji kodi



Kudhibiti viashiria hatarishi





Kufungamanisha miradi ya kipaumbele katika uzalishaji



Sekta isiyo rasmi kujumuishwa



Tathmini na ufuatiliaji



Kudhibiti uchakachuaji mazao

Mchango uchumi mashirika ya umma



Mali bila maelezo kuhojiwa

# Askofu Malasusa akemea ukatili wa kijinsia, awapa kazi wanawake

UK. 3

MICHEZO PANGA SIMBA KUWAKUTA HAWA UK.24 | MAONI, KATUNI UK.6

## Taharuki kuvunjika daraja Dar, Bagamoyo

**Na Elizabeth Zaya**

DARAJA la Mpiji linalounganisha Mkoa wa Dar es Salaam na wilaya ya Bagamoyo mkoani Pwani, juzi lilizua taharuki kwa abiria na madereva baada ya magari kukwama katika foleni takribani saa nane kutokana na hitilafu kujitokeza na kusababisha kufungwa.

Nipashe ilishuhudia foleni kubwa ya magari yaliyokuwa yakitokea Dar es Salaam kwenda Bagamoyo na yale yaliyokuwa yakitoka mikoa mbalimbali kuingia Dar es Salaam.

Daraja hilo ambalo ni kiunganishi kikubwa cha mikoa hiyo, lilipata tatizo upande mmoja baada ya mvua zinazoendelea kunyesha kutikisa kingo zake.

Beatrice Mushi, mkazi wa Bunju, alisema alikutana na adha hiyo wakati akitokea Bagamoyo kurudi Dar es Salaam.

"Licha ya kutoka mapema Bagamoyo, nimefika nyumbani usiku wa kuamkia leo (jana) majira ya saa 8:00 za usiku. Na hapo ni baada ya kuamua kupita njia ya Kibaha," alisema Mushi ambaye ni jirani ya mwandishi wa habari hii.

Baadhi ya madereva wa daladala za Bagamoyo - Bunju B, walisema kuanzia asubuhi mpaka saa 10:00 jioni, walipita vizuri eneo hilo lakini saa moja baadaye, ndipo ilipobainika daraja hilo limetoboka na kufungwa.

Mmoja wa madereva hao, Mahadhi Rajabu, alisema alipata taarifa kuwa hali ni mbaya katika eneo hilo majira ya saa 12:00 jioni akiwa anakaribia darajani hapo na alipofika eneo la Baobab, akalazimika kuwashusha abiria ili watembee.

"Nilipanda gari tukaanza kuondoka, lakini mbele dereva akapewa taarifa na mwenzake kuhusu tatizo lililotokea katika daraja la Mpiji, hivyo tukashuka na kuanza kutembea," alisema Caren Mashimba.

"Ninaishi Kerege, lakini shughuli zangu ninafanyia Bunju B, kwa hiyo leo (jana) ilinibidi niamke kuja kibaruani, kwa hiyo nililazimika kupanda gari mara mbili," aliongeza.

Dereva mwingine, aliyejitambulisha kwa jina la Victor, alisema wakati daraja hilo linafungwa, alikuwa Bunju B akisubiri kupakia abiria lakini hakufanya hivyo.

Dereva wa bajaji, William Christopher, alisema hitilafu iliyotokea katika daraja hilo imemsababishia hasara kwa kuwa amekuwa akichukua abiria wa Kerege na Mapinga kuwapeleka Bunju B na abiria huchangia huduma hiyo mpaka Sh. 1,000 kila mmoja.

"Ninaishi Mapinga, shughuli zangu ni Mapinga-Bunju na kwa siku ninaweza kwenda zaidi ya ruti 10 lakini juzi hali ilikuwa mbaya. Tulilazimika kuegesha bajaji, niliacha Bunju nikavuka darajani kwenda nyumbani kwa bodaboda," alisema.

Kutokana na adha hiyo, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, Kamanda wa polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Wahandisi wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni na viongozi wa mkoa wa Pwani, walikesha eneo hilo kuhakikisha matengenezo yanafanyika na huduma kurejea.

Akizungumza usiku huo katika eneo la tukio, Chalamila alisema daraja hilo limepata hitilafu kutokana na mvua inayoendelea kunyesha, hivyo kutikisa kingo zake.

Mkuu wa Wilaya ya Bagamoyo, Halima Okash, aliwahakikishia wananchi kwamba wanafanya kazi kuhakikisha daraja hilo linarejea katika hali yake kwa wakati. Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, alisema tayari amewasiliana na TANROADS pamoja na viongozi wa mikoa hiyo miwili ili daraja hilo lirejee katika hali yake.

Bashungwa aliagiza Mtendaji Mkuu wa TANROADS kupitia mameneja wake, kufanya tathmini ya sasa ya madaraja na barabara ili kuhakikisha hakukatiki mawasiliano ya miundombinu hiyo wakati mvua ikiendelea kunyesha. Wakati jitihada za matengenezo na kurejesha daraja hilo katika hali yake ya kawaida zikiendelea, jana magari yaliruhusiwa kupita kwa awamu upande mmoja.



Mwenyekiti wa Chama cha Wakala wa Utalii Tanzania (TATO). Wilbard Chambulo, wa pili kutoka kulia, akikabidhi misaada mbalimbali kwa Serikali kwa ajili ya waathirika wa maporomoko ya tope katika baadhi ya vijiji vya Hanang mkoani Manyara. Misaada hiyo ni pamoja na mabati 4000, maji ya kunywa tani 37,800 na tani 10 za unga wa ngano. Misaada hii ni sehemu ya michango ya wanachama wa TATO. **PICHA:MPIGAPICHA WETU.**

## Vipaumbele vinane Dira Maendeleo 2050

**Augusta Njoji na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan ametaja maeneo manane yanayopaswa kupewa kipaumbele katika mchakato wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050, huku akiagiza ukusanyaji maoni uzingatie ushirikishwaji wa wadau wote.

Maeneo hayo ni pamoja na mwelekeo wa uwekezaji na usimamizi wa maboresho ya kiutendaji wa mashirika ya umma, maadili ya taifa kwa kuwa na jamii yenye ujasiri wa kuhoji wanaojipatia mali wasio na maelezo nazo.

Katika uzinduzi wa mchakato wa ukusanyaji maoni ya dira hiyo jana jijini hapa uliokwenda sambamba na maadhimisho ya miaka 62 ya Uhuru wa Tanganyika, Rais Samia alitaja mchango mdogo wa mashirika ya umma katika kukuza uchumi licha ya juhudi zinazochukuliwa na Msajili wa Hazina.

"Dira mpya iweke mwelekeo wa uwekezaji na usimamizi wa maboresho ya kiutendaji wa mashirika ya serikali ili yaongeze ufanisi katika uendeshaji na kuhimili ushindani," alisema.

Pia alisema tathmini inaonyesha nchi imepiga hatua katika kuweka uwazi na kusimamia maadili ya utumishi wa umma na kwamba ili kudumisha hilo, lazima kuwe na jamii yenye ujasiri wa kuhoji wanaojipatia mali bila maelezo, inayochukia rushwa, inayojituma bila kusukumwa, kupinga uchakachuaji wa mazao kama pamba na korosho na kuongezwa mawe, pamoja na kulaani ukwepaji kodi.

"Tujenge jamii yenye maadili. Sina shaka suala hili litapewa uzito mkubwa kwenye mijadala ya kuandaa dira mpya na kuangalia ni kwa namna gani serikali na taasisi zisizo za serikali, ikiwamo za kidini, zitakavyochangia kujenga maadili. Misingi hii itajenga jamii bora na kuvutiwa na wengi kuja Tanzania kufungua fursa," alisema huku akiagiza dira hiyo izingatie ukuaji wa uchumi kufungamanishwa na sekta za uzalishaji kikiwamo kilimo.

"Kwenye kilimo nchi yetu imefanya kazi nzuri. Sasa Tanzania tunajitosheleza kwa chakula kwa asilimia 124 na huku tukielekea asilimia 140 ifikapo mwaka 2025. Suala lilillo mbele yetu ni masuala ya lishe na usalama wa chakula,"alisema huku akibainisha dira mpya iweke lengo la kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha uzalishaji wa chakula kwa ajili ya Afrika na dunia.

Pia alisisitiza kipaumbele kupata takwimu kwa sekta isiyo rasmi kwa kuwa inawezekana katika eneo la kukuza uchumi imefanyika kazi kubwa, lakini kutokana na kutokuwa na takwimu, wamejikita kwenye sekta rasmi.

Kadhalika alitaka kufikiriwa namna ya kuchochea ukuaji wa uchumi kwenye maeneo ya uzalishaji yanayowagusa wananchi wengi zaidi na yanayotengeneza ajira.

"Eneo la tatu, ni tathmini na ufuatiliaji ambalo kwa kiasi kikubwa huko nyuma hatukulipa umuhimu mkubwa. Tuliagizwa kufanya tathmini na ufuatiliaji kila mwaka lakini tumefanya mara moja tu. Tungefanya tathmini kila baada ya muda tungebaini viashiria mapema na kurekebisha na kwenda vizuri zaidi," alisema.

Alitaja eneo lingine kuwa ni utaratibu wa kufungamanisha miradi ya kipaumbele kwa sekta zinazohusika kwenye uzalishaji.

"Eneo lingine ni kubaini viashiria hatarishi na kuweka udhibiti. Uzoefu wa dira ya mwaka 2025 unaonyesha kumekuwa na matukio makubwa ya kimazingira kama El-Nino, ukame, maradhi, vita vya kikanda ambavyo vimekuwa nje ya uwezo wetu mambo haya yakitokea yanaathiri utekelezaji wa mipango ya maendeleo.

Alisema inapoandikwa dira mpya, matukio makubwa ya kidunia ambayo yanaweza kuathiri utekelezaji wake hivyo, yabainishwe na kuzingatia matukio ya dharura yanayoibuka duniani na nchini pamoja na kujadili mbinu za kukabiliana nayo.

"Taasisi za sekta binafsi za ndani zinatakiwa kuwa na uwezo na utayari wa kupokea na kushirikiana na wageni wanaokuja kuwekeza nchini kufanya biashara na kutengeneza ajira kwa wananchi na hatimaye kuchangia ukuaji wa uchumi wetu," alisema.

**MAADHIMISHO UHURU**

Rais Samia alisema miaka 62 inatosha kufanya tathmini ya mapito na kubainisha njia muafaka ya kusonga mbele zaidi.

Aliahidi kuendeleza mema yote yaliyoiletea maendeleo nchi na kujifunza katika vikwazo walivyokutana navyo watangulizi wake.

"Waswahili wanasema usipojipanga kupanga unapanga kupangwa yaani kwa Kiswahili kinachoeleweka usipojipangia utapangiwa, sasa kupangiwa kuna hasara zake. Anayekupangia ndiye anaweka faida zake kwenye mipango anayokupa, lakini ukijipangia unapanga wewe mwenyewe kwa faida zenu wenyewe,"alisema.

**MSAMAHA WAFUNGWA 2,244**

Katika hatua nyingine, Rais Samia ametoa msamaha kwa wafungwa 2,244 ambapo 263 wameachwa huru, wawili waliohukumiwa adhabu ya kifo wamebadilishiwa adhabu na kuwa kifungo cha maisha huku 1,979 wamepunguziwa sehemu ya adhabu zao ambazo wataendelea kuzitumikia gerezani.

Kwa mujibu wa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni, wafungwa walionufaika ni waliohukumiwa kifungo kuanzia miaka miwili na kuendelea ambao wametumikia robo ya adhabu zao gerezani walioingia kabla ya Oktoba 12, 2023.

Pia alisema wafungwa wenye magonjwa ya kudumu au sugu, wafungwa wa maisha ambao wametumikia vifungo vyao kwa miaka 15 na kuendelea, wafungwa wa kunyongwa waliomaliza taratibu za kimahakama na wamekaa gerezani kwa miaka 10 na kuendelea wamebadilishiwa adhabu na kwenda kifungo cha maisha.

Msamaha huo pia alisema wafungwa wazee wenye umri wa miaka 70 au zaidi, walioingia na ujauzito, wenye ulemavu wa mwili na akili, waliohukumiwa adhabu ya kuwekwa kizuizini ambao wamekaa gerezani kuanzia miaka 10 au zaidi.

## HABARI KITAIFA

# Bodaboda zaonywa kubeba wanafunzi

**Na Steven William,** MUHEZA

JESHI la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani wilayani Muheza, Tanga, limepiga marufuku wanafunzi chini ya miaka minane kupakiwa kwenye bodaboda wakati wakienda shule na kurudi nyumbani.

Mkuu wa Kikosi wilayani humo, Leonard Bandola, alitoa onyo hilo wakati akizungumza na walimu, wazazi na walezi wanaosomesha watoto wao katika shule ya msingi binafsi ya Chogogwe wilayani hapa.

"Sisi ndio wasimamizi wa sheria za usalama barabarani, inakataza kumpakia mtoto kwenye pikipiki aliye chini ya miaka minane ili kulinda usalama na afya yake na hii ni kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafirishaji Ardhini (LATRA) iliyoanzishwa mwaka 2010 na kuanza kufanya kazi rasmi 2011", alisema Bandola. Alisema katika kusimamia sheria hiyo, wanalazimika kutumia busara zaidi kwa kuwa kila wanapotaka kumsimamisha dereva wa bodaboda naye huongeza mwendo.

Alisema kuacha kumfukuza hasa anapokuwa amepakia mtoto au watoto kwa kuwa anaweza kupata ajali kwa mwendo kasi na kusababisha hatari zaidi kwa afya, ulinzi na usalama wa mtoto ni busara za jeshi hilo.

Bandola alisema kuwa kupitia utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto ipo haja kwa wadau wote wakiwamo wazazi, walezi, walimu na mamlaka zingine kuunganisha nguvu kukomesha suala hilo.

Alisema kumpakia mtoto mwenye umri huo kushuka chini kwenye bodaboda sio tu ni kinyume cha sheria, bali ni hatari kwa afya kwake.

Pia alisema kiafya mtoto anayebebwa kwenye pikipiki bila kuwa na nguo nzito za kumsitiri baridi na upepo njiani anaweza kupata magonjwa ya njia ya hewa ambayo tiba yake inaweza kugharimu fedha nyingi.

"Ninatoa wito kwa wazazi na walezi kuangalia uwezekano wa kuanza kutumia usafiri mwingine mbadala kama vile magari ya shule yaliosajiliwa kubeba watoto kuanzia chini ya miaka minane ili kulinda afya na usalama wao" alisema.

Pia alikumbusha kwenye mabasi ya shule ambayo hajayasajiliwa na kupakwa rangi ya njano kuwa ni hatari kwani inapotokea ajali wanafunzi watakaopata majeraha hawatalipwa.

# Dk. Malasusa akemea ukatili wa kijinsia, awapa jukumu wanawake

**Na Restuta James**

ASKOFU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Mashariki na Pwani (DMP), Dk. Alex Malasusa, amekemea ukatili wa kijinsia na kuwataka wanawake kushiriki katika vita hivyo ili haki ipatikane kuanzia ngazi ya familia.

Askofu Malasusa ambaye pia ni Mkuu Mteule wa KKKT, aliyasema hayo jana Dar es Salaam wakati wa ibada ya maadhimisho ya Krismasi iliyoandaliwa na Umoja wa Wanawake wa Dayosisi hiyo, yaliyofanyika katika Usharika wa Temboni.

Dk. Malasusa alisema baadhi ya watu wanafanya ukatili kwa watoto kwa kudanganywa na waganga kwamba watapata utajiri wa haraka, jambo linalonyonga haki na kuongeza dhuluma katika jamii na ukatili dhidi ya kundi hilo.

"Nina hakika chochote kitakachoungwa mkono na wanawake kama hili la kupinga ukatili wa kijinsia, litafanikiwa haraka sana. Nimeshukuru sana kuona mnaungana na watetea haki wengi duniani kuhakikisha haki inasimama na dhuluma zinaondolewa," alisema.

Askofu Dk. Malasusa alisema dhuluma inapozidi, nchi inaingia gizani na kwamba Mungu hafurahishwi na taifa lisilo na haki.

"Tumesikia matendo mengi ya aibu yenye kuumiza mioyo jinsi watoto na wanawake wanavyonyanyasika. Tunaliweka taifa katika hali mbaya," alisema.

Dk. Malasusa alisema maadhimisho ya Krismasi ni ishara ya ujio wa Yesu Kristo ambaye ni amani na haki ya dunia, hivyo ni muda wa watu kujitathmini na kufuata injili inayohubiri upendo wa Mungu kwa wanadamu.

"Jambo la kusikitisha ni kwamba wanaofanya ukatili tukisikia majina yao unaona wako wanaoenda kanisani," alisema.

Awali, Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa DMP, Veronica Lyanga, alisema wanawake wa KKKT wanaungana na serikali na wadau wengine kukemea vitendo hivyo.

"Tumeamua kupaza sauti zetu kukemea unyanyasaji na ukatili unaotendwa kwa wanawake, watoto na wanaume. Vitendo hivi ni kinyume na neno la Mungu kwenye Mithali 14:34 inayosema 'Haki huinua taifa bali dhambi ni aibu ya watu wowote," alisema.

Viongozi wa Umoja wa Wanawake wa Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT), Mkoa wa Dar es Salaam, Neema Massawe na Dosca George, walitoa rai kwa dini zote kuungana katika kupinga ukatili, ili makundi yote katika jamii yaishi kwa amani, usawa na haki. Katika maadhimisho hayo, wanawake walifanya maandamano mafupi yaliyopokewa na Askofu Malasusa, wakiwa na mabango yanayopinga vitendo vya ukatili.

Maadhimisho hayo yalihudhuriwa na zaidi ya wanawake 500 pamoja na wachungaji, wainjilisti na watenda kazi (ma-Parishi Worker)



Ofisa Uhusiano Mwandamizi wa AICC, Frederick Maro (wa pili kushoto), akimkabidhi sehemu ya msaada kwa waathirika wa maafa Katesh Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga (wa pili kulia). Kulia ni Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Bunge, Sera na Uratibu), Dk. Jim Yonazi, na kushoto ni Katibu Tawala wa Mkoa wa Manyara, Karoline Mthapula. **PICHA: FARAJ MSALA.**

# Waathirika wa mafuriko Katesh walia hali ngumu

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

WAATHIRIKA wa mafuriko na maporomoko ya tope ya Mlima Hanang, wamesema maafa yaliyowapata yamewaacha katika hali ngumu kimaisha, hivyo kuiomba jamii kuwashika mkono ili warejee katika hali ya kawaida.

Kutokana na maafa hayo, serikali ilitangaza kutoa misaada mbalimbali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali yenye thamani ya Sh. bilioni 2.5 huku hadi juzi misaada kutoka kwenye taasisi mbalimbali ikiendelea kutolewa. Serikali pia kupitia kwa Rais Samia Suluhu Hassan ambaye alikwenda Katesh Alhamisi wiki hii, iliahidi kuwapa viwanja vya makazi waathirika.

Mkazi wa Katesh, John Thomas, akizungumza na Nipashe akiwa katika kambi ya waathirika iliyoko Shule ya Sekondari Katesh, alisema wakati maafa yanatokea alikuwa safarini Dareda, wilayani Babati, hivyo alikuta nyumba yake imezolewa na hana kitu chochote.

"Mimi mnavyoniona hapa sina kitu chochote. Ni hizi nguo nilizovaa na sijui hata mifugo yangu na ndugu zangu waliko," alisema Thomas.

Mkazi mwingine, Amina Musa, alisema maafa yamemwachia umaskini kwa kuwa bidhaa zake zote za nafaka alizokuwa anauza zilisombwa na maji. Kutokana na athari hizo, aliomba serikali impatie mtaji ili aendelee na maisha.

Mkazi wa Katesh, Liydia Petro, alisema maafa yalisomba nyumba yake lakini alifanikiwa kuwaokoa watoto wake. Alisema wakati mafuriko yanatokea, alifikiri kuna radi inapiga mahali ndipo alitoka na kuona tope na akakimbia na familia yake.

**MICHANGO YAMIMINIKA**

Kutokana na maafa hayo yaliyosababisha vifo vya watu 80 na wengine 133 kujeruhiwa, misaada kutoka taasisi mbalimbali imeendelea kutolewa kwa waathirika.

Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la World Vision Tanzania, James Anditi, alisema baada ya kusikia maafa hayo, wamechangia Sh. milioni 30.5 ili kuwasaidia waathirika kupata chakula, maji na matibabu.

Anditi aliishukuru serikali kwa namna ilivyolishughulikia janga hilo na shirika lake liko tayari kuunga mkono. Alisema walipokwenda kijiji cha Gendabi, walibaini wananchi wamepoteza mali zao huku watoto na wanawake wakiwa wameathirika pakubwa.

Mkurugenzi huyo alisema wamebaini watoto na wanawake wameanza kupata tatizo la afya ya akili, hivyo wanatakiwa kupewa ushauri nasaha na kuahidi kuendelea kufanya utafiti juu ya tukio hilo ili kuona namna ya kuwasaidia waathirika.

**MUHIMBILI YAJITOSA**

Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) imetoa msaada wa dawa na vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. milioni 38 kwa ajili ya kusaidia waathirika wa tukio hilo.

Kwa mujibu wa taarifa yake kwa vyombo vya habari, msaada huo umelenga kusaidia jitihada za utoaji huduma katika eneo hilo, ambalo hivi karibuni lilikumbwa na maafa ya mafuriko yaliyosababisha vifo na majeruhi na uharibifu wa mali na miundombinu.

Mkuu wa Idara ya Famasia, Mfamasia Nelson Faustine, akizungumza kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, alisema sambamba na msaada huo, Muhimbili imetuma msaikolojia tiba kuungana na timu za wataalam walioko huko wanaotoa huduma kwa waathirika wa mafuriko hayo.

Taarifa pia ilisema bodi ya wadhamini, menejimenti na wafanyakazi Muhimbili wanaendelea kutoa pole kwa wananchi wa maeneo hayo kutokana na madhara waliyopata.

**AICC YAFARIJI WAATHIRIKA**

Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC) kimetoa msaada kwa waathirika waliokumbwa na mafuriko na maporomoko ya tope yaliyoisababishwa na mvua kubwa kwenye Katesh.

AICC ilikabidhi msaada wa mablanketi 200 na

Sh. milioni 12 kwa Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga, aliyeambatana na Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Dk. Jim Yonazi, na Katibu Tawala Mkoa wa Manyara, Karoline Mthapula, juzi.

Akikabidhi msaada huo kwa niaba ya Mtendaji Mtendaji wa AICC, Ofisa Uhusiano Mwandamizi, Fredrick Maro, alisema AICC imeguswa na maafa hayo na inatambua wajibu wake wa kuisaidia jamii inayoizunguka.

**Imeandaliwa na Jaliwason Jasson (MANYARA) na Romana Mallya (DAR)**

## AMDT yashauri matumizi ya mbegu zilizoboreshwa

**Na Maulid Mmbaga**

TAASISI ya Kuboresha Mifumo ya Masoko ya Kilimo Tanzania (AMDT) imehamasisha Watanzania kufanya kilimo chenye tija kwa kutumia mbegu zilizoboreshwa zikiwamo za alizeti, jamii ya mikunde na mahindi ili kuongeza mnyororo wa thamani.

Mkurugenzi Mkuu wa AMDT, Charles Ogutu, aliyasema hayo jana jijini Dodoma wakati akifungua mafunzo kwa wanahabari ambayo yanalenga kuwaongezea uelewa kuhusu kazi wanazofanya pamoja na kilimo bora ili waweze kuelimisha jamii.

Alisema sababu kubwa ya kuanzishwa kwa taasisi hiyo ilikuwa ni kutatua changamoto mbalimbali ambazo zimekuwa zikijirudia.

Ogutu alisema viongozi wa kisiasa na wadau wa maendeleo wamefanya jitihada nyingi katika sekta ya kilimo ili kutatua matatizo yaliyopo.

"Pamoja na jitihada hizo mabadiliko bado hayajawa makubwa kama tulivyotarajia, hivyo ikaonekana kuna haja ya kuanzisha taasisi ambayo itatumia mfumo kuangalia matatizo ya kimfumo ambayo yakitatuliwa yanaweza kutupeleka katika mabadiliko ya kweli katika sekta ya kilimo," alisema Ogutu.

Alisema AMDT katika utendaji wao wamejigawa katika misingi miwili, kuchagua mazao ambayo wanaona yana umuhimu zaidi na kutafuta changamoto za kimfumo na namna ya kushirikiana na wadau wengine kuzitatua.

Alisema nguzo ya pili ni kuangalia namna changamoto hizo zikishatatuliwa zinaweza kuwafikia watu wengi zaidi huku wakijihusisha zaidi na mazao ya alizeti, jamii ya mikunde na mahindi.

"Mazao haya yana umuhimu wa kipekee na waziri mwenye dhamana amekuwa akizungumzia ajenda hiyo kila wakati kwamba, ifikapo 2030 tunataka sekta ya kilimo iwe imekua kwa asilimia 10," alisema Ogutu.

Pia alisema programu mbalimbali zinazofanyika kama Jenga Kesho Bora (BBT) ni kuhakikisha ifikapo 2030, sekta ya kilimo inatoka kwenye ukuaji wa asilimia nne hadi asilimia 10.

Alisema wizara ilifanya utafiti uliolenga kuangalia mazao gani yakitiliwa msisitizo yatasaidia kufikia malengo na kuonesha ni ya nafaka, mafuta ya kupikia na jamii ya mikunde.

Alisema ajenda hiyo ilikuja wakati ambao AMDT ilishaanza na bahati nzuri baadhi ya mazao hayo ni ya kimkakati na yako kwenye Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (SDPll).

Alisema katika mazao hayo, alizeti imeorozeshwa kama zao muhimu ambalo linaweza kulisaidia taifa katika kupunguza gharama ya kuagiza mafuta ya kula kutoka nje, na mengine wanayoshughulika nayo yako kwenye mkakati wa serikali.



Mratibu wa Kitaifa wa Mradi wa Urejeshwaji Endelevu wa Mazingira na Hifadhi ya Bioanuai (SLR) unaosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais, Dk. Damas Mapunda, akizungumza wakati wa mafunzo kwa kamati za maliasili na mazingira za vijiji zinazotekeleza Mradi wa Urejeshwaji Endelevu wa Mazingira na Hifadhi ya Bioanuai (SLR) unaosimamiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais kutoka Bonde la Ziwa Rukwa Jijini Mbeya. **PICHA:MPIGAPICHA WETU**

## Mtoto wa Prof. Shaba asilimulia alivyoshuhudia kifo cha babake

**Na Christina Mwakangale**

ANALE Shaba, mtoto wa daktari bingwa mbobezi katika uchunguzi, Prof. James Shaba, amesimulia alivyoshuhudia kifo cha baba yake, kilichotokea nyumbani kwake, Chicago nchini Marekani, kutokana na ugonjwa wa saratani.

Prof. Shaba (88), alifariki dunia Desemba 5, mwaka huu, akiwa amezungukwa na familia yake, wakiwamo binti zake, Anale na Stella. Anatarajiwa kuzikwa Jumamosi ijayo.

Anale kwenye taarifa yake kwa Nipashe, alimwelezea baba yake alivyokuwa na mapenzi kwa nchi yake ya Tanzania, akijituma na kujitoa akiwa daktari bingwa.

"Desemba 5, mwaka huu, nyumbani Chicago IL, Marekani, akizungukwa na dada yangu Stella, nami (Anale), baba yangu alifariki dunia baada ya kupambania uhai wake akiugua saratani.

"Tumepata fursa hii ya kipekee ya amani pamoja na baba (Prof. Shaba) yetu," alisema Anale kwenye taarifa hiyo juzi.

Alisema kazi ya baba yake ya utabibu kwa vitendo, imekuwa kitu cha pili alichokipenda, baada ya upendo usio na kikomo kwa mkewe.

"Elizabeth (Beth) Shaba, walioana na baba miaka 55 iliyopita kabla ya kifo chake mwaka 2018. Kutengana kwao ilikuwa sikitiko kubwa. Kwa maana hiyo, tumeikubali hali hii kwa ugumu kwamba sasa baba atapumzika pembeni mwa mke wake, Beth," alisema Anale.

Kuhusu maziko yanayotarajia kufanyika Desemba 16, mwaka huu, Anale alisema awali kutakuwa na ushiriki wa jamii katika Kanisa la St. James Cathedral 65 E, Mtaa wa Huron huko Chicago IL, siku hiyo.

Anale alisema kumbukumbu ya Prof. Shaba itafanyika pia Tanzania mwakani, katika Kanisa Kuu la Mtakatifu Albano, Dar es Salaam, ili kutoa fursa kwa ndugu, marafiki na jamaa kushiriki kumkumbuka bingwa huyo.

Prof. Shaba aliyezaliwa Aprili 5, 1935, alijizolea umaarufu katika stadi za kuutambua mwili wa binadamu na sababu za kifo na aliitumikia Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Moja ya rekodi zake zinazomtambulisha hadi sasa ni kuchanganua chanzo cha kifo cha aliyekuwa Waziri Mkuu, Edward Sokoine, alityefariki dunia April 12, 1984.

## Hawara adaiwa kuua mama na wanawe wawili kisa mapenzi

**Na Waandishi Wetu**

MAMA na watoto wawili wamefariki dunia baada ya nyumba yao kuchomwa moto na mtu anayesadikiwa kuwa ni hawara wa mwanamke huyo kwa kile kinachodaiwa kuwapo kwa mgogoro wa kimapenzi baina yao.

Mgogoro huo unadaiwa kuhusishwa na uhalali wa baba wa mtoto wa miezi mitano.

Waliofariki dunia ni Eva Stephano (32) na watoto wake, Samwel Simon (3) na Abel Richard mwenye umri wa miezi mitano, ambao ni wakazi wa Mtaa wa Lwanima, wilayani Nyamagana, Mwanza.

Tukio hilo lilitokea Desemba 7, 2023, majira ya saa 6:30 usiku katika nyumba hiyo yenye vyumba vitatu ambamo pia kulikuwamo na watu wengine, Lucy Stephano (25), Lucy Simon (5) na Charity Amos (1) waliookolewa.

Baada ya moto huo kutokea, wananchi kwa kushirikiana na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, walivunja mlango wa nyumba na kuwaokoa watu hao watatu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Wilbroad Mutafungwa, alisema uchunguzi wa awali wa jeshi hilo ulibaini kuwapo kwa chupa za plastiki zenye mabaki ya mafuta ya petroli yanayodaiwa kutumiwa na mtuhumiwa ambaye jina lake limehifadhiwa.

"Imeonekana kuwa kulikuwapo na mgogoro baina ya Eva na hawara wake ambaye kwa sasa jina tunalihifadhi kwa ajili ya uchunguzi. Walikuwa wakigombania mtoto Abel Richard ambaye amefariki dunia katika tukio hilo. Mwanamume huyo anadai mtoto huyo ni wake na Eva akidai ni wa mwanamume mwingine,"alisema Mutafungwa.

Alisema miili ya marehemu imehifadhiwa katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Bugando kwa ajili ya uchunguzi huku wanaodaiwa kuhusika na tukio hilo wakiendelea kutafutwa.

"Mali zote zilizokuwa ndani ya nyumba zimeteketea kwa moto na nyumba imeharibika, hivyo niwatake wananchi kuwa na utaratibu wa kutatua migogoro kwa njia ya amani na kuacha kujichukulia sheria mkononi," alisisitiza Mutafungwa.

Juzi, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla, alifika eneo la tukio kuifariji familia ya marehemu Eva na kuliagiza Jeshi la Polisi kumsaka mtuhumiwa wa tukio hilo anayedaiwa kutokomea kusikojulikana.

"Tukio kama hili haliwezi kuvumiliwa hata kidogo. Polisi fanyeni uchunguzi wa kina hakikisheni mhusika anakamatwa na kuchukuliwa hatua kali za kisheria ili kuzuia matukio kama haya yasiendelee kutokea mkoani hapa," alisisitiza Makalla.

### WATOTO WAFA MAJI

Katika hatua nyingine, Kamanda Mutafungwa alisema watoto wawili wa familia moja Revocatus Behatusi (9) na mdogo wake Japheti Behatusi (7), wakazi wa Mtaa wa Kibera, Bugogwa, wilayani Ilemela, wamefariki dunia kwa kuzama katika Mto Bukindwa wakati wakichunga ng'ombe.

Pia alisema Jeshi la Polisi linawashikilia wanaotuhumiwa kuwa ni matapeli sugu, Andrew John (44) na Deusi Buye (53) Mwenyekiti Mstaafu wa Mtaa wa Ilamba 'A' Nyamhongolo kwa kumtapeli John Nyakyoma (30), mkazi wa Musoma, mkoani Mara, kwa kumuuzia kiwanja namba 198 Block 5 eneo la Nyamhongolo kwa Sh. milioni 13 Septemba 5, mwaka huu, kinachomilikiwa na mtu mwingine.

"Mnunuaji alipohitaji kukiendeleza kiwanja hicho iligundulika kinamilikiwa na mtu mwingine.Tuwaombe wananchi sasa wawe makini na kujiridhisha kutoka katika mamlaka husika pindi wanapohitaji kununua viwanja,"alisema SACP Mutafungwa

**IMEANDALIWA na Thomas Wandiba (SAUT) na Remy Moka (SAUT).**

## HABARI KITAIFA



Balozi wa Tanzania nchini Ujerumani, Hassan Mwamweta (kushoto), akiwasili Ikulu ya Ujerumani na kupokewa na Rais wa Shirikisho la nchi hiyo, Frank Walter Steinmeier, kwa ajili ya kuwasilisha hati za utambulisho. **PICHA: UBALOZI**

# Vijana wafurahia huduma kuwekewa maputo

**Na Romana Mallya**

ZAIDI ya watu 150 wenye uzito uliopitiliza wamejitokeza katika Hospitali ya Taifa Muhimbili-Mlongazila ndani ya mwaka mmoja kuwekewa puto maalumu kwenye tumbo la chakula ili kupungua wengi wakiwa ni vijana kuanzia miaka 25 mpaka 35.

Huduma hizo ambazo zimetimiza mwaka tangu kuanza hospitalini hapo Novemba 8, mwaka huu, zimesaidia kwa kiwango kikubwa kurejesha mwonekano mpya kwa wahusika ambao sasa wanaufurahia.

Zamzam Ismail, ni mmoja wa vijana waliojitokeza kuwekewa puto akiwa na uzito wa kilo 132 na kupungua kilo 34 ndani ya miezi minane baada ya kutolewa.

Katika mitandao ya kijamii kuna video fupi iliyotolewa na hospitali ya Muhimbili-Mlongazila ikionyesha namna Zamzam alivyokuwa awali mwenye umbile kubwa na sasa akiwa na mwonekano mpya.

"Nilikuja kuweka puto Februari, mwaka huu, baada ya kugundulika nina matatizo mbalimbali na kuona uzito wangu ni mkubwa. Nilikuwa nina kilo 132 na wiki iliyopita (Novemba 6, mwaka huu) nimetoa nimekuta nina kilo 98 baada ya kuziona zinanitosha.

"Ninaendelea vizuri, ninaweza kutembea umbali mrefu, ninaweza kufanya shughuli zangu bila kupumua kwa taabu. Ukiwa na uzito mkubwa unashindwa kufanya shughuli zako. Ninawashauri wenye uzito mkubwa wanaweza kuweka puto kwani halina madhara, halisumbui," alisema mwanamke huyo.

Zamzam alisema anaendelea kula kiasi cha chakula ambacho alikuwa akila akiwa na puto kwa kuwa anajiona bado analo.

Katika mahojiano maalum na mwandishi wa habari hii wiki iliyopita, Mkuu wa Idara ya Upasuaji Muhimbili-Mloganzila, Dk. Eric Muhumba, alisema kati ya waliojitokeza kuwekewa puto, idadi kubwa ni wanawake huku wanaume wakiwa ni asilimia 10 tu.

Alisema waliojitokeza katika huduma hiyo wengi ni vijana kuanzia umri wa miaka 25 mpaka 35 na kufuatiwa na kundi la pili lenye umri wa miaka 35 mpaka 45.

Dk. Muhumba anabainisha kwamba, asilimia 90 ya waliowekewa puto walikuwa na mafanikio makubwa na asilimia 10 walipata changamoto mbalimbali wakiwamo wenye vidonda vya tumbo ambao walitoa puto mapema.

"Kuna mwingine anawekewa puto lakini anajikuta anapungua kidogo, kuna mmoja tumemtoa juzi (wiki iliyopita) baada kama miezi 10 na amepungua kilo 10 tu ambayo hayakuwa matarajio yetu. Alikuwa kimya na alipokuja tulipomtoa amepunguza kilo hizo tu, hivyo kwa sasa anafanya utaratibu mwingine.

"Sana sana huwa tunawatoa mapema kwa wale wanaopata maumivu ambao ni wachache kati ya waliojitokeza. Baada ya kuwahudumia hawa, na kupata matokeo mazuri watu wanaendeela kujitokeza, Zamzam alitolewa puto mwezi Novemba," alisema.

# China yamwaga vifaa maabara utafiti uvuvi

**Na Mwandishi Wetu**

CHINA imetoa msaada wa vifaa vya maabara kusaidia utafiti katika Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI).

Hayo yalibainishwa na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Daniel Mushi, baada ya kupokea ugeni kutoka China ulioongozwa na Makamu wa Rais wa Chuo cha Sayansi cha China (CAS), Prof. Wang Keqiang, katika kikao kilichofanyika katika ofisi za wizara zilizoko Temeke Veterinari, Dar es Salaam.

Katika kikao hicho, Prof. Mushi alipokea taarifa ya msaada wa vifaa vya maabara vyenye thamani ya Dola za Marekani 190,000 (zaidi ya Sh. Milioni 575.9 ) kutoka kwa Prof. Zhang Ganlin, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Jiografia na Limnolojia ya Nanjing (NIGLAS) ambaye ameongozana na Makamu wa Rais wa CAS.

Akipokea taarifa hiyo kabla ya kushuhudia utiaji saini mkataba wa kuimarisha ushirikiano katika ulinzi wa mazingira na usimamizi wa rasilimali zilizoko kwenye maji, makubaliano ambayo yanatengeneza fursa nyingine ya kuendeleza utafiti na sayansi, Prof. Mushi alisema CAS na NIGLAS zinashirikiana na TAFIRI katika kuendeleza utafiti wa uvuvi.

Alisema taasisi hizi zimefanya miradi ya pamoja mitano na zimetoa machapisho tisa ya kimataifa ambayo yameongezea mwonekano TAFIRI na Tanzania, kufundisha wanafunzi tisa wa shahada ya uzamili na shahada ya uzamivu, kuwezesha maabara za utafiti za TAFIRI kwa ajili ya kufanya utafiti wa viumbe maji na uvuvi katika Ziwa Tanganyika na ukanda wa Bahari ya Hindi.

"Kutokana na maendeleo ya sayansi na technolojia ambayo China imeyafikia hadi sasa, Tanzania tunaona tunafaidika sana kushirikiana na taasisi mojawapo ya utafiti ya China na leo (Alhamisi) Makamu wa Rais wa CAS ambayo inasimamia taasisi zingine zaidi ya 160 za utafiti China, amekuwapo nasi na ametuhakikishia wataendelea kutoa rasilimali nyingi kwa Nanjing Institute of Geography and Technology ili kuendeleza ushirikiano wao na TAFIRI.

"Sisi kama nchi tunamuona China kama rafiki wa kweli. Hata Mwalimu (Julius) Nyerere (Rais wa Kwanza wa Tanzania) aliwahi kusema 'tunao marafiki wengi lakini China ni rafiki wa kweli na huhitaji kuwa mkomunisti ili ujue kwamba China ana mambo mengi ya kutufunza kuhusu maendelelo'. Kwa hiyo, kwa niaba ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi tunawashukuru sana wenzetu wa China kwa ushirikiano wao wa kweli na kwa kutushika mkono ili kutunyanyua tuweze kufikia hatua ya maendeleo ambayo wao wameweza kufikia," alisema Prof. Mushi

Prof. Wang alisema wako tayari kushirikiana na Tanzania katika kukuza uchumi wa buluu, hasa kuongeza nguvu katika tasnia ya ukuzaji viumbe maji katika maji chumvi, upande wa bahari.

Alisema ushirikiano uliopo kati ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Sayansi na Teknolojia ya China kupitia NIGLAS na TAFIRI una zaidi ya miaka 15 na ulijikita zaidi kwenye maziwa makuu na maji baridi mengine nchini.

Pia alisema pamoja na kuwa makubaliano katika ya Wizara ya Sayansi na Teknolojia ya China na Wizara ya Mifugo na Uvuvi yanatoa nafasi ya kukuza sekta ya uvuvi nchini, watawekа mkazo zaidi kwenye tasnia ya ufugaji viumbe maji wa baharini kutokana na msisitizo aliouonyesha Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alipokutana nao katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Dar es Salaam.

Prof. Wang aliongeza kuwa kwa sasa wana taasisi 124 zenye ubobezi tofauti katika sayansi na teknolojia zenye zaidi ya watumishi 70,000 wa kada mbalimbali na wengine zaidi ya 800 wanaounda 'think tank' ya China kwenye masuala ya sayansi, teknolojia na ubunifu.

## Ujerumani yaahidi kukuza ushirikiano na Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**

UJERUMANI imeahidi kuendelea kushirikiana na Tanzania katika nyanja mbalimbali za kimaendeleo ikiwa ni mwendelezo wa kudumisha uhusiano baina ya nchi hizo.

Hayo yalisemwa juzi na Rais wa Shirikisho la Ujerumani, Frank Walter Steinmeier, wakati wa hafla ya kupokea hati za utambulisho za Balozi wa Tanzania nchini Ujerumani, Hassan Mwamweta, kwenye Ikulu ya Ujerumani.

Rais Steinmeier alisema serikali yake inaunga mkono jitihada za maendeleo zinazotekelezwa na serikali ya Tanzania chini ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Tanzania na Ujerumani zinashirikiana kwenye maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa miradi ya afya, elimu, utunzaji wa mazingira, utamaduni, uhifadhi wa mazingira, utalii, biashara; uwekezaji na kubidhaisha Kiswahili.

Rais Steinmeier alifanya ziara ya siku tatu nchini Tanzania kuanzia Oktoba 30, maka huu, akiwa ameambatana na ujumbe wa makampuni mbalimbali kwa ajili ya kuangalia fursa ili kuwekeza nchini.

Akiwa nchini alifanya mazungumzo na mwenyeji wake, Rais Samia kuhusu mambo mbalimbali ya ushirikiano kati ya Tanzania na Ujerumani kwa manuufaa ya pande zote mbili.

## Wahitimu JKT wapewa bil. 1.8/- programu BBT

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imetoa Sh. bilioni 1.8 kwa ajili ya vijana wa Programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora (BBT) waliohitimu mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) ili kuendesha kilimo.

Akifunga mafunzo hayo juzi kwa vijana 688, Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alisema fedha hizo zitatumika kuanza kilimo kwa ajili ya kurudisha kile walichopewa na serikali.

"Fedha ziko tayari kwa ajili ya mradi wa BBT, hivyo ninahitaji kuona vijana jitihada zenu zinasonga mbele, serikali imejipanga kuhakikisha mnapiga hatua katika kilimo,"alisema.

Bashe aliishukuru JKT kwa mafunzo waliowapa vijana hao na kueleza kuwa awamu nyingine ya Program ya BBT itaanzia JKT kabla ya kuja uraiani.

Mkuu wa JKT, Meja Jenerali Rajabu Mabele, alisema programu hiyo imekuwa ya viwango vya juu, hivyo vijana wanapaswa kuzingatia walichofundishwa.

"Tumefurahi sana kupata vijana hawa wa mafunzo, tunasubiri awamu nyingine ili tuwape mafunzo na nidhamu kwenye kilimo,"alisema Jenerali Mabele.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wanawake washike hatamu mapambano ukatili kijinsia

**VITENDO** vya ukatili wa kijinsia hasa kwa wanawake na watoto, vimekuwa vikishamiri siku hadi siku na kusababisha taifa kuingia doa kutokana na matukio yanayotendeka kama vile ubakaji, ulawiti, ukeketaji, ndoa za utotoni na vipigo dhidi ya wanawake.

Matukio hayo pia yamesababisha watoto wa kike kukatisha ndoto zao za kimaisha kutokana na mila kandamizi zinazoendelea katika baadhi ya maeneo kama vile kulazimishwa kuolewa kutokana na tamaa za wazazi wao pamoja na kubakwa, hivyo kupata mimba zisizo tarajiwa.

Licha ya kutungwa kwa sheria kali na baadhi ya watu wanaopatikana na hatia kufungwa maisha au miaka 30 jela, vitendo hivyo vimekuwa vikiongezeka siku hadi siku. Sababu kubwa ni baadhi ya watu katika jamii kuendekeza ushirikina kwa kuamini kuwa kubaka au kulawiti ni njia mojawapo ya kupata utajiri.

Baadhi ya wazazi na walezi pia wamekuwa chanzo cha kuota mizizi kwa matukio hayo kwa sababu ya kushindwa kuripoti matukio kama hayo ambayo mengine hufanywa na watu wa ndani ya familia au kumalizana nje ya mahakama na watuhumiwa kwa kupewa fedha au mali.

Jana, Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Mashariki na Pwani (DMP) kupitia Umoja wake wa Wanawake, lilifanya maadhimisho ya Krismasi yaliyohusisha zaidi ya wanawake 500 katika Usharika wa Temboni na ujumbe mkubwa uliotolewa ni kushamiri kwa vitendo vya ukatili wa kijinsia na watoto katika jamii.

Kutokana na kukithiri kwa vitendo hivyo, Kiongozi wa Dayosisi hiyo, Askofu Dk. Alex Malasula alikemea na kuweka wazi mambo hayo yanavyolifedhehesha kanisa na taifa kwa ujumla. Askofu Malasusa aliweka bayana kwamba vitendo hivyo vinalichafua kanisa la Mungu kwa kuwa miongoni mwa watu wanaotuhumiwa au kupatikana na hatia ya kufanya ukatili huo ni wenye majina ya Kikristo.

Bila kuuma maneno, alisema ni wakati sasa wa kanisa kusimama kidete na kukemea vitendo hivyo kwa kuwa havina viashiria vizuri kwa maendeleo na ustawi wa kanisa, jamii na taifa kwa ujumla. Alisisitiza kwamba ili kukomesha vitendo hivyo, wanawake wana nafasi kubwa kutokana na historia yao hata katika maandiko matakatifu.

Kwa umuhimu huo, kiongozi huyo aliwatwisha mzigo wa mapambano dhidi ya vitendo hivyo kwa kupaza sauti na kukemea vitendo hivyo na maovu yanayofanyika katika jamii huku akibainisha kuwa kama watatekeleza wajibu huo, kuna uwezekano mkubwa kwa mambo hayo kutoweka na hata hatua dhidi ya wahusika kuchukuliwa.

Ni kweli wanawake kama wanavyoelezwa kuwa ni 'jeshi kubwa', wana nafasi kubwa katika kuhakikisha ukatili katika jamii unakomeshwa. Hiyo inatokana na ukweli kwamba nchini Tanzania, walioibua wazo la kuanzishwa kwa sheria ya makosa ya kujamiiana ni wanawake na kuna ushuhuda mkubwa inavyotekelezwa kwa wanaokutwa na hatia kupewa adhabu kali.

Wanawake, ni dhahiri kwamba wana nafasi kubwa katika kuongoza mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia na vitendo viovu vinavyotokea katika jamii. Kupitia mikusanyiko yao kama VICOBA, makongamano ya kidini, vikundi vya ujasiriamali na maeneo ya kazi, wanaweza kuanzisha programu na mada ambazo zinaweza kuchochea mapambano dhidi ya vitendo hivyo.

Historia inaonyesha kwamba katika harakati za mapambano ya utetezi wa haki katika jamii, wanawake wamefanikiwa katika mipango hiyo na kwa asilimia kubwa ustawi, maisha, usawa wa haki za binadamu zimechangiwa kwa kiasi kikubwa na wanawake. Hata katika hili la ukatili wa kijinsia linawezekana kupata mafanikio makubwa kama wanawake watakuwa mstari wa mbele na kushika hatamu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Miaka 62 ya uhuru, hivi ndivyo Nyerere alivyotaka nchi ya uchumi wa viwanda?

**JANA** ilikuwa Desemba 9, Watanzania waliungana kuadhimisha miaka 62 ya uhuru wa iliyokuwa Tanganyika uliopatikana 1961 baada ya kuwa chini ya ukoloni uliowafanya wakose uhuru wa kujiamulia mambo yao wenyewe.

Miaka 62 ya uhuru si haba kwani kipindi hicho chote wananchi wameendelea kudumisha umoja, mshikamano na amani, huku baadhi ya nchi zimekumbana na mitafaruku mbalimbali.

Nimegusia kidogo lakini lengo langu ni kutaka kujadili, jitihada za Rais wa kwanza Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alizofanya kwenye sekta ya viwanda ili kuinua uchumi wa nchi.

Wakati nchi inapata uhuru mwaka huo, historia inaonyesha kuwa sekta ya viwanda ilikuwa changa kwa kuwa kulikuwa na viwanda vichache ambavyo vilikuwa vikichangia asilimia 3.5 ya Pato la Taifa (GDP) na kuajiri asilimia tisa ya ajira zote.

Baada ya kushika uongozi, Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliamua kuweka mkakati wa kuendeleza viwanda ikiwa ni sehemu ya mpango wa kwanza wa miaka mitano mwaka 1964. Historia inaonyesha kuwa mpango huo ulitoa kipaumbele kwa sekta ya kilimo, kwa ajili ya kuvutia wawekezaji wa ndani kuanzisha viwanda vitakavyozalisha bidhaa zilizokuwa zinaagizwa kutoka nje ya nchi.

Baada ya kuanzishwa kwa Azimio la Arusha mwaka 1967, serikali ilibadili mkakati wa maendeleo ya viwanda uliokuwa unalenga sera ya Ujamaa na Kujitegemea.

Azimio hilo lilijikita katika misingi miwili; kuhakikisha mkakati haulengi katika uwekezaji kwa sekta binafsi na kutaifisha viwanda na mashirika yote yaliyokuwa yanamilikiwa na sekta binafsi.

Kimsingi, Tanzania ni miongoni mwa nchi za Afrika zilizobarikiwa kwa kuwa na rasilimali mbalimbali, yakiwamo madini, mbuga za wanyama, misitu, milima na mabonde, maziwa, mito na ardhi yenye rutuba.

Vilevile, ardhi hiyo inaruhusu kuwapo kwa kilimo cha mazao mbalimbali ya chakula na biashara ambayo yanaweza kusaidia katika shughuli za uzalishaji kwenye viwanda.

Kutokana na umuhimu wa rasilimali hizo, alianzisha viwanda vingi ili kujenga taifa imara linalojitegemea kiuchumi, vilijengwa karibu kila mkoa visaidie kuimarisha uchumi kwa kupata malighafi toka kwa wakulima na kutengeneza bidhaa na kuuza soko la ndani na nje ya nchi.

Baadhi ya viwanda hivyo ni Urafiki Textile, Mwatex, Mutex, Kilitex, Sungura Textile,Tanganyika Packers na UFI, ambavyo kwa sasa ni kama havipo kabisa kwani havizalishi tena.

Vingine ni Morogoro Canivas ambacho kilitengeneza magunia na maturubai, Moro Shoes, Bora Shoes (viatu), huku vya ngozi vikiwa ni MorogoroTanneries na Mwanza Tanneries.

Lakini pia kulikuwa na Kibo Match Factory (vibiriti), National, Matsushita na Philips, vilivyotengeneza betri na redio Pamba Enginenering cha kuchonga vipuri vya mashine za kuchambua pamba.

Nimejaribu kutaja vichache hivyo, lakini ukweli ni kwamba nchi ilikuwa na viwanda vingi ambavyo baadaye vilibinafsishwa miaka ya 90 na sasa vingine vimeshindwa kujiendesha na hivyo kufungwa.

Jitihada za Baba wa Taifa, zililenga kupiga hatua katika maendeleo ya taifa kiuchumi na kuwakwamua Watanzania kutokana na umaskini, lakini baada ya uongozi wake mambo yalibadilika.

Mambo yamebadilika kwa sababu baada ya uwekezaji, baadhi ya viwanda vilipoteza mwelekeo na kusababisha ndoto za Baba wa Taifa za kujenga Tanzania ya viwanda zishindwe kutimia.

Ninadhani tunaposheherekea miaka 62 ya uhuru, tuangalie ni wapi ambapo tumejikwaa hadi kusababisha viwanda vikongwe kufa na kusababisha kundi kubwa la Watanzania kukosa ajira.

Nakumbuka kuna kiwanda kimoja ambacho Rais wa awamu ya tano, hayati Dk. John Magufuli aliwahi kusema kuna mwekezaji alikichukua badala ya kukiendeleza, anakitumia kufugia mbuzi wake.

Hivyo, ingekuwa ni vyema kama serikali itaangalia viwanda ambavyo walipewa wawekezaji na kushindwa kuviendesha, wapewe wengine ili vifanye kazi na kuwezesha Watanzania kupata ajira.

Si vibaya kuangalia ni wapi ambapo kama nchi tumejikwaa hadi kusababisha viwanda vikongwe kufa na kusababisha kundi kubwa la Watanzania kukosa ajira, ili lifanyiwe kazi.

SAFU

## FIKRA MBADALA

# Janga la Katesh ni la kitaifa, CCM, CHADEMA, sare za nini?



Pascal Mayalla

WATANZANIA ni watu wamoja kwenye shida na raha, kwa tabu na matatizo. Kunapotokea majanga ya kitaifa kama lile lililowakumba ndugu zetu wa Katesh, Hanang mkoani Manyara, tunakwenda kuwafariji waathirika na sare za chama cha siasa ili iweje?.Tunataka kuwaonyesha waathirika kuwa chama chao kinawajali sana?

Kwanza, niungane na Watanzania wote kutoa pole zangu za dhati kwa waathirika wa janga hilo la mafuriko Katesh. Pole sana kwa waliopoteza maisha. Nawatakia uponyaji wa haraka walio hospitalini na utengamao wa haraka kwa waliopoteza makazi, nyumba na mali. Poleni sana kwa yote.

Pia nitoe pongezi kwa serikali ya mkoa wa Manyara chini ya Mkuu wa Mkoa, mwanamke wa shoka, Queen Cuthbert Sendiga, na serikali kuu ikiongozwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa, mawaziri, makatibu wakuu, watendaji wote na wananchi wa Katesh kwa hatua za awali za kukabiliana na janga hili.

Shukrani za pekee na pongezi za dhati ni kwa Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye amekatisha ziara yake nje ya nchi na kurejea nyumbani kuwafariji wafiwa na kuratibu uokozi na utengemao kwa karibu. Baada ya kurejea na kukagua maeneo yaliyoathirika, Rais Samia aliwahakikishia wakazi wa mji mdogo wa Katesh walioathirika na mafuriko kuwa serikali itarejesha huduma zote za msingi za kijamii na kusisitiza kuwa itaendelea kufanya tathmini ya uharibifu wa mali.

Sambamba na hilo, aliiagiza Wizara ya Nishati kuangalia uwezekano wa upatikanaji wa umeme wa dharura baada ya miundombinu kuharibika kutokana na maafa hayo ili shughuli za uopoaji zifanyike usiku na mchana.

Vilevile, Rais Samia alitaka tahadhari zote za msingi zichukuliwe ili kusitokee janga lingine la mlipuko wa magonjwa, hivyo kuheshimu kanuni za usafi kwa kuwa majanga wakati mwingine huzua maradhi kama kipindupindu. Kwa hiyo Rais Samia ameielekeza Wizara ya Maji kuhakikisha huduma za maji safi na salama zinaendelea kupatikana muda wote huu hususan maeneo yaliyowekwa kambi za kusitiri waathirika wa janga hilo.

Mafuriko mazito yaliyotokea yamesababisha vifo vya Watanzania 80 hadi juzi, huku kaya 1,150 zikiwa zimeathirika na watu 5,600.

Pia kumekuwa na majeruhi takriban 117 pamoja na uharibifu wa miundombinu ya barabara, maji na umeme.

Kutokana na majanga ya asili kama ilivyotokea Katesh, nina mambo mawili. La kwanza ni kwanini baadhi ya viongozi wanakwenda na sare za vyama vyao? Wananchi wa kawaida au wanachama, wanaweza kuvaa vyovyote zikiwemo sare za vyama, maana kwa umaskini wetu kwenye baadhi ya maeneo ya vijijini, nguo nadhifu pekee walizo nazo ni sare za vyama. Lakini kwa viongozi kuvaa sare za vyama kwenye shughuli za kitaifa, haijakaa vizuri.

Kwenye matukio ya Katesh, nimeona baadhi ya viongozi wa vyama na wanachama wao, wamevaa sare za vyama vyao katika hali inayoonyesha waliambiana na kujipanga ili 'kutokelezea' kivyama.

Huku ni kuyafanya matukio ya kitaifa kuwa ya kisiasa na kuyahusisha na siasa za matukio, kwa lugha ya Kiingereza wanaita "politicizing everything".

La pili, je, hatuwezi kuwafanyia utafiti watu wa makabila ya Wabarbaig, Wahadzabe, Wataturu, Wasandawe na Watindinga huwa wanajuaje kutatokea majanga ya asili (natural disasters) na kukimbia eneo hilo kabla ya majanga hayajatokea?

Mlima Hanang uko kwenye safu ya milima ya volcano kama Oldonyo Lengai, usikute una volcano hai!. Enzi zile Oldonyo Lengai, ulipofuka moshi mzito na majivu yale yaliwaathiri wanyama na mifugo. Ya kufungwa ndiyo iliathirika kutokana na kufungiwa lakini wanyama wa porini walijua na walikimbia kabla.

Watu wa makabila ya wawindaji wa asili, Watatu, Wasandawi, Wabarbaig, Wahadzabe na Watindiga, pia wana 'natural seismology intelligence', hivyo wana uwezo huo kwa kuwasikia wanyama pori, wakiwaona wanakimbia kwenda upande fulani, nao hukimbia. Baada ya kukimbia, ndipo huko nyuma hutokea la kutokea.

Tusiwategemee sana wazungu na utafiti wao na vifaa vyao. Tufanye utafiti wa haya makabila ya wawindaji wa asili kujua wanatumia nini na viashiria gani kuyakimbia maeneo kabla majanga hayajatokea?

Kwa mujibu wa mashuhuda, walisikia mlipuko kama wa volkano usiku wa manane na hali kama ya tetemeko la ardhi, ndipo ikanyesha mvua kubwa Mlima Katesh na kusababisha maporomoko ya udongo yaliyosombwa na mafuriko na kuzisomba nyumba za wakazi wa chini ya mlima.

Mashuhuda hao wanasema mpaka kunakucha walikuwa bado wanaona mvuke ukipaa juu kutoka Mlima Katesh.

Kutokana na imani za kiasili, simulizi zinasema kuna watu wana nguvu na uwezo wa ajabu ama kusababisha majanga au kudhibiti majanga. Mkama Rumanyika wa Karagwe, alikuwa akiwapiga maadui zake kwa mvua ya mawe na kumrarua kiongozi wao kwa kumpiga radi.

Hizi zote ni sayansi za kiasili za Kiafrika. Zikifanyiwa utafiti zitalisaidia sana taifa letu. Mnaonaje kama tutafanya utafiti kwenye hili?

**Mungu inusuru Hanang,**
**Mungu Ibariki Tanzania.**
**Paskali**
**+255 754 270403**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Viongozi wetu, mchezo wenu, majanga kwetu



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

**Ninalomwunga mkono Ulimwengu ni lile la ziara kuachiwa wananchi waanike hasi na chanya zao kwa mkuu wao wa nchi huku wakuu wa mikoa na wilaya wakibaki kutoa ufafanuzi na kujibu maswali ya kwa nini hasi hizi na kupongezwa kwa chanya zao.**

MWEZI jana, nilimsikia mwanahabari nguli, mwanasheria mbobevu na mwanasiasa galacha nchini, Twaha Khalfan au Jenerali Ulimwengu, nikamwelewa barabara kwa kauli yake kuhusu uongo!

Katika kauli yake hiyo, alikuwa akizungumzia kile kinachoitwa uteuzi wa rais na jinsi wateule wanavyopatikana, hasa akihoji kama kweli marais wanapofanya uteuzi, huwa wanawajua barabara wanaowateua.

Alitolea mfano wa Tanzania, ambako mathalan rais huteua wakuu wa wilaya zaidi ya 120 au wakuu wa mikoa wapatao 30, akitanabaisha kuwa ni kweli baadhi ya watu hao rais huwa hawajui na wala kupata kuonana nao.

Lakini huwasilishiwa majina na wasaidizi wake, wakimwaminisha kuwa wanafaa hivyo atie saini tu kuwa hao ndio hasa wanaoweza kumsaidia katika majukumu yake ya kuongoza nchi.

Ni kweli si rahisi akawajua wote. Baadhi huwateua bila kuonana nao uso kwa uso.

Akasema mathalan, wakuu wa mikoa hukutana nao baadhi siku anawaapisha na kushangaa "ahaa kumbe wewe ndiye fulani!" Na akishawaapisha basi hutawanyika mikoani kwao, kuanza majukumu ya kumsaidia.

Ulimwengu akasema, siku rais anapofanya ziara mkoani, hukutana na mteule wake huyo ambaye humsomea taarifa ya mkoa na hata kwa kumdanganya, huku akimpamba rais na kumwambia yaliyo chanya mkoani mwake na kuacha yaliyo hasi.

Baaada ya hapo, rais atapanda gari na mkuu wa mkoa kwenda wilayani ambako nako watamkuta mkuu wa wilaya naye kama bosi wake wa mkoa, atampamba rais na mkuu wa mkoa na kisha kumwaga chanya tupu na kuficha hasi huku wananchi wakishangilia.

Wakishamaliza ziara kila mtu hurejea alikotoka na vyombo vya habari kuripoti chanya zilizomwagwa na wakuu hao mbele ya mamlaka ya uteuzi, huku wananchi wakibaki na hasi zao zikiwaumiza rohoni kila kukicha, kana kwamba hawana viongozi wawakilishi wa rais.

Ninalomwunga mkono Ulimwengu ni lile la ziara kuachiwa wananchi waanike hasi na chanya zao kwa mkuu wao wa nchi huku wakuu wa mikoa na wilaya wakibaki kutoa ufafanuzi na kujibu maswali ya kwa nini hasi hizi na kupongezwa kwa chanya zao.

Tunashuhudia wananchi wanavyohangaika na kuhangaishwa na mikoani na wilayani mwao na wakifanyiwa hivyo na viongozi wao ambao ni wawakilishi wa rais, waliotarajiwa kufanya mema kwao lakini inakuwa tofauti.

Yanatokea matatizo na kero ambazo zingeweza kuzuiwa, lakini hilo halifanyiki mpaka ziara ya rais ndipo yatasikika kama si kwenye mabango basi risala (kama zitapewa fursa) za wananchi, ndipo mkuu wa nchi ambaye hawezi kufika kila kona ya nchi, anapofumbuka macho.

Mfano mdogo tu, ni wa juzi kati hapa, Novemba 29 pale Manyoni, Singida. Basi la Ally's Star lilipogonga treni na kusababisha vifo vya watu 15 na zaidi ya majeruhi 30, kitu kilichoonekana ni mwendokasi aliokuwanao dereva wa basi hilo.

Kwa kawaida inapotokea ajali kama hiyo, siku zote gari au binadamu huwa ndiye mkosaji aliyefuata njia ya reli na kugonga treni, hivyo haishangazi kusikia binadamu kagonga treni na ndiye mwenye makosa. Ndivyo ilivyotokea kwenye basi hilo lililokuwa likitoka Dar es Salaam kwenda Mwanza.

Mara tu baada ya mzinga huo kutokea, kama ilivyo ada, viongozi walifika mara moja kushuhudia tukio na kutoa matamko yaleyale ya kuhadharisha dhidi ya mwendo kasi na madereva kuwa waangalifu, na kutoa maagizo ya papo kwa hapo, ambayo mengi huanza na kuishia hapo.

Nakumbuka alifika Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Jumanne Sagini, na kutoa pole kwa waliopatwa na kadhia hiyo, lakini akaja na tamko la kuhakikisha eneo hilo la makutano ya reli na barabara, linawekwa kizuizi na tuta.

Kwamba treni inapokaribia eneo hilo, basi kizuizi kishuke na kuzuia barabara ili magari yasimame na kupisha treni kupita, halikadhalika tuta liwezeshe gari kupunguza mwendo. Yaani hadhari kabla ya hatari.

Unajiuliza kirahisi tu, hivi kabla ya ajali hiyo hakuna viongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA) waliopata kupita hapo na kuona hatari hiyo? Hakuna viongozi wa Shirika la Reli Tanzania (TRC) waliopita hapo na kuona uwezekano wa ajali kama hiyo kutokea?

Walishapita na kuona, ila lazima kwanza litokee la kutokea, ndipo tupate akili ya nini kifanyike na kwa wakati gani. Ila uzuri wetu ni wepesi na wenye haraka ya kusahau. Hivi mnakumbuka amri ya kuzuia mabasi kuingia vituo vya mafuta kujaza yakiwa na abiria? Nani anatii? Mpaka kilipuke ndipo tutarudia historia. Mungu tubariki.

# CWP yaweka mkakati kuongeza idadi ya wanawake katika uongozi

**Na Romana Mallya**

WABUNGE Wanawake wa Jumuiya ya Madola (CWP) wamekutana kuweka mikakati ya kuhakikisha wanawake wanakuwa na uwezo na ujuzi wa kushiriki na kushindana katika michakato ya uchaguzi na kuwa sehemu ya ngazi za uamuzi.

Akifungua mkutano wa wabunge vinara wa masuala ya kijinsia juzi jijini Dar es Salaam ambao zaidi ya nchi 30 zimewakilishwa na matawi yote ya CWP, Waziri wa Maliasili na Utalii, Angellah Kairuki, aliyemwakilisha Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, alisema umelenga kuangazia masuala ya usawa wa kijinsia.

Waziri Kairuki alisema dira ya mkutano huo pia, ni kuangalia kwa namna gani mabunge kama chombo cha uwakilishi yanazingatia mlengo wa usawa wa jinsia.

"Mabunge yetu na miundombinu na miundo yake yamewekа mazingira gani kuhakikisha wabunge wanawake wanaweza kuendelea na majukumu ya uzazi.

"Pili, ukiangalia suala zima la uwakilishi, wanapewa nafasi kiasi gani kuwakilisha wanawake wenzao bungeni, sheria, sera na kanuni je, kuna vikwazo gani vinafanya wanawake washindwe kushiriki katika nafasi za siasa na uongozi na katika ngazi za uamuzi," alisema.

Kairuki alisema Australia kwa miaka 170 imepata uwiano wa kijinsia katika bunge lake wa asilimia 50/50 na katika ngazi ya Baraza la Mawaziri wamefikia wanawake asilimia 67 na wanaume asilimia 33.

Alisema kwa upande wa Rwanda wanawake wabunge ni asilimia 61 na Tanzania imefikia asilimia 37 kuelekea asilimia 40.

"Tanzania tunaamini kwa kuwa na Rais mwanamke, kwa kuwa na Spika mwanamke ambaye pia ni Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), kwa hakika mkutano huu umekuja muda muafaka na tuna sheria mbalimbali za uchaguzi.

"Ninadhani miswada yake ipo tayari itakwenda kuangaliwa kwa milengo hii kuhakikisha pia katika sheria za uchaguzi zinavyoendeshwa kwa mlengo kwa kijinsia ukoje, ili kutoa nafasi kwa wanawake wengi kushiriki nafasi za kisiasa," alisema.

Pia alisema kwa Tanzania kuna machapisho mawili ya mkakati wa kuhakikisha wanafikia mlengo wa kijinsia katika Bunge na mkakati na uongozi mzima.

"Usawa wa kijinsia katika siasa unaweza kupatikana tu ikiwa wanaume watafanya kazi bega kwa bega na wanawake kushiriki wajibu katika kuvunja mila na desturi zenye madhara, pamoja na vikwazo vya kitaasisi, kimuundo na kisheria vinavyozuia ushiriki wa wanawake katika siasa sawa na wenye ushawishi," alisema.

Alisema ni muhimu kuweka mazingira ambayo yanawezesha ushiriki wa wanawake katika siasa katika ngazi zote za uamuzi.

"Bunge linalozingatia jinsia ni Bunge linalojibu mahitaji na maslahi ya wanaume na wanawake katika miundo, uendeshaji, mbinu na kazi zake," alisema waziri.

Alisema katika kuzingatia masuala ya kijinsia, pamoja na mambo mengine, mabunge yanapaswa kupitisha mkakati wa kuzingatia kijinsia ambao utasaidia kuimarisha na kuhamasisha taasisi kusaidia ushiriki sawa na wenye maana wa wanawake katika mabunge ya CPA.

Mwenyekiti wa WCP Kanda ya Afrika, Ndangaiza Madina, alisema inahitaji dhamira thabiti ya kisiasa, uongozi makini, juhudi za makusudi za kupitisha na kutekeleza sera na kufanikisha jambo hilo.

"Kuna haja ya kuwa na mifumo ya kisheria na programu za mabadiliko ya kijinsia, kuendeleza ushirikiano wa kimkakati na kushirikisha wadau wote muhimu wakiwamo wanaume na wanawake kuelekea maono ya pamoja ya kuunda jamii jumuishi," alisema.

Katibu wa Mabunge wa Jumuiya ya Madola Kanda ya Afrika (CPA) na Katibu wa Bunge la Tanzania, Nenelwa Mwihambi, alisema usawa wa kijinsia siyo tu kwamba ni suala la haki za kimsingi za binadamu bali pia, ni sharti la maendeleo endelevu na maendeleo ya kijamii.

Alisema ni kwa ushirikiano na kubadilishana mawazo ambapo nchi zinaweza kukuza masuluhisho ya kiubunifu na mikakati ya kuendeleza usawa wa kijinsia katika jamii.




Mshauri Mkuu wa mikakati wa Benki ya Biashara na Maendeleo ya Mashariki na Kusini mwa Afrika (TDB), Catherine Kimaryo (wa pili kulia), akizungumza wakati wa mdahalo wa mkutano wa Kimataifa wa wafanyabiashara wanawake barani Afrika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Wengine ni Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Alaska, Jeniffer Bash (kulia), Mkuu wa kitengo cha mikopo midogo wa benki ya NMB, Linda Teggis (kushoto) na Mkurugenzi wa Kampuni ya Youlead, Sodfa Daaji. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# TIRA yaagizwa kuboresha mifumo madai bima

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imeitaka Mamlaka ya Usimamizi wa Bima (TIRA), kuendelea kuboresha mifumo ya kushughulikia madai na malalamiko ya wateja pamoja na kuongeza elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kukata bima.

Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema hayo juzi kwenye hotuba yake iliyosomwa na Waziri wa Michezo, Sanaa na Utamaduni, Dk. Damas Ndumbaro, wakati wa uzinduzi wa Ripoti ya Soko la Bima mwaka 2022.

"Si kwamba mifumo ya kushughulikia madai haipo, ipo lakini bado ufanisi bado ni mdogo bali nataka muwe na mifumo itakayoondoa kabisa urasimu na kutoa matokeo ndani ya muda mfupi.

Mtu aliyekata bima akilalamika kwamba amepata janga lakini hajalipwa kwa wakati, watu wote wanaosikia malalamiko hayo wanakuwa na mtazamo hasi kuhusu bima," alisema.

Alisema ili kuondoa mtazamo hasi dhidi ya bima ni lazima TIRA iweke mikakati madhubuti ya kuyashughulikia madai na malalamiko ya wateja kwa wakati na kwa ufanisi ili kuvutia watu wengi kujiunga na huduma za bima.

"Kwa takwimu tulizosikia hapa tangu mwaka 2018 hadi 2022 kama zilivyotangazwa na Mkurugenzi Mkuu wa TIRA zinaonyesha kwamba sekta ya bima inakuwa kwa kiwango kizuri sana lakini ukiona unakua usishangilie sana unapaswa kujizatiti usirudi nyuma na badala yake ukue zaidi ili mchango wa bima usaidie kukuza uchumi," alisema

Alipongeza TIRA kwa kuamua kuweka wazi ripoti hiyo kwani imesaidia wadau wengi nchini na dunia nzima kwa ujumla kufahamu mwenendo wa bima nchini na mchango wake kwenye ukuaji wa pato la taifa.

Dk. Ndumbaro alisema ripoti hiyo imetokana na hatua mbalimbali ambazo TIRA inazichukua na kwamba katika kuandaa ripoti hiyo imeongozwa na mambo mbalimbali kama mpango mkuu wa maendeleo wa sekta ya fedha wa 2019-2029.

Alisema wadau wote wanapaswa kuunganisha nguvu na kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa bima kwani watanzania wengi kwa sasa wanajua bima ni kwa ajili ya magari pekee na wengi hawakati bima ya nyumba na thamani zingine wanazomiliki.

"Wengi wanakata bima kwenye magari kwa sababu ya kuogopa kukamatwa na askari wa usalama barabarani lakini askari asingekuwepo wala wengine wasingehangaika kukata bima sasa hii ina maana kwamba uelewa wa umuhimu wa bima na bidhaa zake bado mdogo sana tunatakiwa kutoa elimu zaidi.

## Pinda ataka maboresho uendeshaji vyuo ardhi

**Na Munir Shemweta,** TABORA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geofrey Pinda, amemwelekeza Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Mhandisi Anthony Sanga, kuunda timu maalum ya kufanya tathmini kwa vyuo vya ardhi vya Tabora na Morogoro na kushauri namna bora ya kuboresha vyuo hivyo.

Pinda ametoa agizo hilo juzi wakati wa Mahafali ya 41 ya Chuo cha Ardhi Tabora (ARITA) yaliyofanyika chuoni hapo mkoani hapa.

"Wizara inakwenda kuandaa timu maalum kuja kufanya upya mapitio ya vyuo vyetu vya ardhi ikiwamo makusanyo ya ndani ili kupima uwezo wa mapato ya ndani," alisema Pinda.

Katika kuhakikisha hilo linatekelezwa, alitoa siku saba kuanzia juzi kuundwa kwa timu hiyo haraka itakayofanya ukaguzi wa hesabu, makusanyo ya mapato ya ndani na kutoa ushauri na mambo mengine namna bora ya kutumia mapato ya ndani kwa miradi ya maendeleo.

Pia timu hiyo itaangalia suala la ajira kwa watumishi na kwa mujibu wa Naibu Waziri, vyuo hivyo vinatumia wastani wa Sh. milioni 80 hadi 100 kwa walimu wa muda pekee kiasi alichosema ni kikubwa.

"Katika vyuo vyetu walimu wa muda kwa muhula wanatumia takriban Sh. milioni 80 hadi 100 kwa muhula mmoja. Kiasi hiki ni kikubwa tunaweza kuajiri walimu na sehemu ya watumishi na kupunguza uhaba wa watumishi unaokabili vyuo," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya ARITA, Dk. Lucy Shule, alimweleza Naibu Waziri kuwa chuo kinakabiliwa na upungufu wa watumishi, vyumba vya madarasa, maabara na vyumba vingine vya mafunzo.

"Tunaiomba wizara kuongeza majengo ya maabara ya uchoraji, uchapishaji na kompyuta, hii inatokana na ukweli kuwa mojawapo ya nguzo za ubora wa mafunzo kwa vitendo ni ubora wa maabara na vifaa vinavyotumika," alisema.

Kwa mujibu wa mwenyekiti huyo, ubora wa wahitimu na mafanikio ya wanafunzi unategemea ubora wa programu na kozi walizozisoma pamoja na mchakato wa mafunzo kwa vitendo waliyoyapitia.

Aliiomba wizara kukiongezea chuo vitendea kazi vya kujifundishia alivyoesma vitawasaidia wanafunzi kupata ujuzi na stadi zilizolengwa katika mafunzo yao na kuwawezesha kuwa na umahiri katika kufanya kazi zao kwa kujiamini na ubora unaokidhi viwango vya mahitajio ya soko.

Katika mahafali hayo, wahitimu 1,132 wametunukiwa astashahada na stashahada katika fani za usimamizi wa mazingira, mifumo ya taarifa za kijiografia, sanaa, ubunifu na uchapishaji, urasimu ramani na usimamizi wa ardhi, uthamini na usajili.

# MAISHA

DESEMBA 10, 2023

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*



Ukurasa 14


## Mayai chakula rahisi na kitamu

## MAISHA NI NYUMBA



Ukurasa 15

Epuka nyumba yako kutitia baada ya muda mfupi kwa kufanya haya




## KATUNIKA

Ukurasa 16




# TARABUSHI INAVYOPENDEZA

Ukurasa 13


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| T | ■ | U | M | E | M | E |
| A | ■ | ■ | ■ | N | ■ | N |
| N | ■ | M | E | E | ■ | D |
| E | D | A | ■ | Z | E | E |
| S | ■ | N | O | A | ■ | L |
| C | ■ | D | ■ | ■ | ■ | E |
| O | G | E | N | I | ■ | A |


## FUMBO TOTO




Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

SAA, NIA, RAI, LOA, UHURU, ELEWA, UMANA, LISHE, NYERERE, USHAMBA

## AMSHA AKILI





## TOA TOFAUTI 5



## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA

Watoto wawili walikuwa wakigombea mapera, mama mmoja alitokea na kuwaamulia na kuwataka kila mmoja kusema tatizo ambalo limewafanya kugombana.

Juma: John ndiye mgomvi alinipora mapera yangu

John: Hapana yeye ndiye mgomvi alichukua mapera katika mti aliopanda baba

Juma: Ule mti umejiotea pale msituni, huyu ni muongo

Mama: Nyinyi wote nawaona mnadanganya ugomvi haufai kwa sababu huleta chuki

John: Kweli mama hata mwalimu alisema heri nusu shari, kuliko shari kamili

SWALI

Je sukari inayotumika nyumbani inatengenezwa kutokana na zao gani?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Lete mtoto uliyezaa nje kabla sijakuoa nimsomeshe, hutaki!

KARIBU msomaji wangu tuendelee kuchambua vituko duru la Maisha Ndivyo Yalivyo. Ukiona watu wanapita barabarani wanacheka au hawacheki, huko majumbani mwao ni vituko vitupu!

Leo tujadili watoto wanaozaliwa kabla ya wazazi wao kuoana. Na wanapoletwa au kutokuletwa kwenye ndoa, yanakuwapo maswali gani? Yupi anakuwa na uhalali kufanya hivyo?

Imekuwa desturi kwamba baadhi ya kinababa ndio wanaowaletea watoto wa nje ya ndoa wake zao lakini hukumbana na vizingiti vinavyowafanya wafungue midomo na kueleza yanayowasibu kwa upande wao.

Hebu msikie huyu kupitia ujumbe mfupi simu ya kiganjani, kisha tujadili.

"Mimi naitwa JF, nina mke na watoto wawili niliozaa na huyu mama ninayeishi naye. Pia huyu mama ana mtoto wa nje. Hata mimi nina mtoto wa nje ambaye nilimpata kabla sijamuoa. Tatizo ni kwamba nikimwambia amlete yule mtoto aje asomee kwangu anakataa, ila yeye anataka huyo mtoto wangu mimi niliyezaa nje aje na siyo huyo wa kwake.

"Kingine anabagua ndugu zangu ila mimi sifanyi hivyo. Tumeitisha vikao vingi sana kuhusu jambo hili mpaka tumechoka. Je, nifanyeje?" (JF Shinyanga).

Mpenzi msomaji, bila shaka umemsikia mwenzetu huyo kuhusu yanayomsibu. Yako maswali kadhaa ambayo nilipenda kumuuliza JF lakini kwa bahati mbaya simu yake kila nikipiga inaniambia 'samahani mteja unayempigia hapatikani kwa sasa'.

Lengo langu ni kumuuliza maswali yafuatayo; Je, kwa nini anang'ang'ania mtoto huyo wa mkewe aliyemzaa nje aje hapo amsomeshe? Kwani huko aliko hasomi? Na je, huyo wake aliyezaa nje mbona hajamleta hapo nyumbani?

Nauliza hivi kwa sababu anasema amezaa na mama huyu anayeishi naye watoto wawili na wala hasemi anao watoto watatu akiwamo huyo wa nje.

Sasa kama hata huyo wa kwake hajamleta hapo nyumbani, ni kwanini anasisitiza huyo wa mkewe aje amsomeshe wakati ana baba yake? Nini hasa kinachomfanya ang'ang'anie hilo? Ningempata kwa simu angenipa majibu ya maswali yote haya na mengine.

Mpenzi msomaji, hawa jamaa inaonekana walipendana na kuamua kuishi pamoja hata kubahatika kuzaa watoto wawili. Japokuwa kila mmoja alikuwa na mtoto aliyezaa kwingine. Uzuri hapa ni kwamba kila mmoja hakumficha mwenzake.

Binafsi nadhani huyu mama anayo sababu ya msingi ya kutomleta pale mwanae huyo aliyezaa kabla. Huyo mtoto ana baba yake na inawezekana katika kushindwana kuishi pamoja, mama huyu alimkabidhi baba yake au ndugu zake.

Kingine mbona baba huyu yeye hajamleta huyo mwanae wa nje? Mimi nadhani ikiwa hao watoto huko waliko wanapatiwa malezi mazuri, hakuna sababu ya kuwaleta pale.

Kinachotakiwa ni wazazi hawa kuwa na mawasiliano nao kwa maana ya kuwajulia hali, kujua maendeleo yao na pia kuwapa mahitaji stahiki kwa ajili ya makuzi yao eneo la afya, elimu, mavazi na kadhalika.

Hiyo itawasaidia watoto hao kutopoteza uasili wao kwa maana ya kuwajua mama na baba yao mzazi. Watoto hao wanaweza kuletwa hapo wakajichanganya na wenzao halafu wakavurugwa wasijitambue.

Huko wanakoishi, walishazoea aina fulani ya maisha. Walizoea mazingira ya wale wanaowatunza. Watakapoletwa hapo na kuchanganyika na wenzao, inawezekana wasifurahie.

Watoto hao wenyewe kwa wenyewe wataanza kuchunguzana, kusomana na wakati mwingine wakishatambua kuwa huyu ni wa mama na huyu ni wa baba wanaweza kuanza kubaguana. Saikolojia ya watoto ina mitego mingi.

Cha msingi mama akiletewa watoto kama hawa aweke busara mbele katika kuwalea kwa upendo bila kumbagua yule wa mumewe ambaye pale anajikuta yule siyo mama yake mzazi.

Bila kuonyesha mapenzi zaidi kwa mtoto huyu wa nje, uwezekano wa kujisikia mpweke ni mkubwa hasa kwa kuzingatia kuwa bado angali mdogo. Kama ni mkubwa mwenye akili za utambuzi hali inaweza kuwa tofauti.

Ubaguzi wa watoto katika jamii ni kero kubwa. Na hili limeainishwa vema katika Sera ya Maendeleo ya Mtoto Tanzania toleo la 2 la Machi 2008 ambapo tamko la sera linasema;

Serikali kwa kushirikiana na wadau wanaoshughulikia masuala ya watoto ihamasishe wazazi, familia na jamii kuwapatia watoto wote malezi na makuzi sawa.

***Je, una kisa, maoni? Tuma ujumbe mfupi kupitia 0715268581***

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi



# Unamkosea hausigeli, dhihaka ya nini sasa?

KUNA watu wanajua kuigiza maisha. Si lazima uwe sawa nao ila unaweza kujitofautisha nao.

Usiigize maisha na usiishi maisha ya mtu mwingine. Siku ambayo utashtuka na kuanza kuishi maisha yako, utakuwa umechelewa.

Naiona shida kwa wanawake wenye ndoa na 'single mother', ambao wanakimbizana usiku na mchana kutafuta shilingi ili maisha yaende lakini wanasahau wana watoto au waume zao.

Kutafuta pesa sawa ni jambo moja, malezi ni jambo la pili. Lakini mbona sasa ninyi wanawake mlioko kwenye ndoa na 'single mother', mmeinua mabega na kusahau majukumu yenu ya msingi?

Hausigeli akijua unamheshimu na kumpenda, atakuheshimu pia. Atawapenda watoto wako, familia yako na atajali zaidi akidhani yuko kwao, kumbe kuna siku ataondoka na ataanza maisha yake na yeye kama wewe.

Mwanamke aliyeolewa au 'single mother' yeyote, ni lazima ajitambue na aweke kwenye akili yake kwamba matunzo ya mume na watoto wake ni majukumu yake.

Wewe 'single mother' au mke, jiongeze ujue mumeo ni mume wa aina ipi. Ukishajua aina ya mume wako, jipange kukabiliana na aina ya familia uliyo nayo kwa kutoa huduma, kama mama ili uendane na saikolojia ya mumeo.

Ni hivi! wewe mama mwenye familia au wale 'single mother', ni muhimu kujua, kuajiri house girl, hakuondoi au kupunguza wajibu wako kama mama wa familia na kwa mume wako.

Kitu unachotakiwa kuwa nacho akilini mwako kila wakati, ni kujitambua kwamba wewe ndo mlinzi wa mme wako katika mazingira yanayoweza kuonekana kumvutia.

Saikolojia yako, itamsaidia mumeo kuhamishia umakini wake kwako au ukosee ama kujisahau, ahamishie kwa house girl au mdogo wako wa kike.

Hakikisha unasoma mazigira ya mumeo, kujua vitu anavyopendelea na mazingira anayoyafurahia.

Sasa, mbona ninyi wengi wenu, nawaona mkiwakosea sana house girl? hebu punguzeni majivuno basi! Halafu dhihaka ya nini.

Yaani, saikolijia hiyo mmeikosa, na mmeicha inachangamkiwa na kutumiwa na hausigeli. Kwa nini, baba asichepuke kwa sababu anavutiwa nae?

Lile somo la zamani la wanawake waliofundwa wakafundika, la kushuka na kuwa mnyenyekevu kwa mume, kumthamini na kumhudumia hasa hasa kama mke limeishia wapi?

Mnaposema mila kandamizi zinawaathiri wanawake, mnamaanisha na hili pia? au tuanze upya kupambana na mmonyoko upi wa maadili, kati ya ukatili wa kijinsia na udhaifu wa ndoa na matunzo ya familia?

Kumkaimisha hausigeli majukumu hayo yote hadi kufua nguo za ndani za mumeo, kutandika kitanda, kumuandalia mume kifungua kinywa, kumpikia na kufanya usafi chumba unacholala ni kukaribisha matatizo.

Si kosa kama hausigeli atapika chakula cha familia au cha baba kwa sababu inategemea wakati huo, mama yuko wapi, anafanya nini, muda wake wa kuwahi kurudi kupika na kula na familia, ni saa ngapi.

Lakini mazoea na tabia waliyojiidhinishia baadhi ya wanawake walioolewa au single mother, ndiyo tatizo la msingi ninalolizungumza hapa.

Ni makosa makubwa, kutengeneza mazoea ya kila siku chakula cha familia kuandaliwa na hausigeli.

Mwanamke mjanja, wakati yuko bize, huwa anahimiza chakula cha familia kiandaliwe, na ana hakikisha kabla hakijapelekwa mezani, anajiridhisha kama kitamfaa na mume wake.

Lakini anapopata nafasi ya kuandaa chakula, anajitahidi kutulia na kumuandalia mumewe kitu kizuri zaidi ya anavyoandaa house girl.

Narudia tena! ni makosa makubwa hausigeli kuwa 'mkali' wa mapishi kukuzidi mama mwenye nyumba au 'single mother'.

Ukiona mambo yanazidi unga, rafiki tafuta walimu wa mapishi, ingia kwenye mtandao, tafuta namna ya kupika mahanjumati ya kumfurahisha baba au wanao.

Iko siku isiyo na jina, utashangaa hausigeli huyo huyo umempa nafasi ya kukung'oa na yeye akatawazwa rasmi kuwa mama mwenye nyumba.

Hakuna mume mjinga. Jamaa huwa anaona, anajua ni kwa namna gani mwenzi wake, yuko na majukumu mengi.

***•Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa barua pepe: ghandsome79@gmail.com na simu ya mkononi: +255 715 545 490***







Baadhi ya harusi watoto hutumika kama sehemu ya kunogesha sherehe. Pichani ni baadhi ya mavazi yaliyobuniwa kiasili kwa ajili ya watoto wakati wa sherehe za harusi.



# MITINDO





## TARABUSHI INAVYOPENDEZA

KOFIA za Tarabushi ni vazi lenye historia ndefu katika jamii ya Pwani ya Afrika Mashariki.

Mpaka sasa kuna watu wachache ambao wanaendelea kuvaa kofia za tarabushi zile zenye muundo wa kale.

Hata hivyo, kofia hizi zimebadilishwa kimuundo kutokana na mabadiliko yanayoonekana katika sekta ya mavazi.

Kofia za kale zenye rangi nyekundu na inanogeshwa na shada ya nyuzi nyeusi.

Kwa kiingereza zikijulikana kama 'Fez', kwa lugha ya kiarabu inaitwa 'Tarboosh' na waswahili wanaita Tarabushi.

Historia ya Tarabushi, ilianzia tangu dola ya Ottoman ilipotangaza kofia hizo kuwa vazi rasmi kama utambulisho wa himaya hiyo.

Umaarufu wa kofia hizi kwa nchi za Afrika Mashariki ulikuja baada ya ujio wa ukoloni ambao waliunda majeshi na askari wake walitumia kofia za tarabushi kama vazi rasmi.

Hata hivyo, vijana wa sasa wamebadilisha mwonekano ili ziendane na wakati na pia matamanio ya wengi.

Tarabushi zilizoboreshwa hazina shada la nyuzi na badala yake kunawekwa pambo mbele au kutokuwa na alama yoyote.

Mara nyingi kofia za Tarabushi za kileo zinavaliwa na suti maalum ya kitambaa zenye muundo wa Kaunda Suti au nguo za kitamaduni zilizobuniwa kisasa.



UREMBO

Na Mary Geofrey

# Furahia nywele zenye afya

TATIZO la kupoteza nywele sio hali ya kawaida, ingawa kuna sababu nyingi lakini kubwa inatokana na madhara ya moja kwa moja ya kiafya.

Hali hii inatokana na maumbile kama usawa wa homoni, vimelea vya ngozi ya kichwa, mkazo, magonjwa ya 'Autoimmune' na utapiamlo.

Njia ya kutunza

Kuna dawa za asili ambazo unaweza kutumia kukuza nywele zako.

Pia njia ya kusugua ngozi ya kichwa, ambayo kutumika kwa mafuta ya nywele na maski, hufufua ngozi ya kichwa na kuboresha afya ya nywele.

Kutumia mafuta ya Alovera kutibu tatizo hilo, husaidia kupunguza ngozi ya kichwa na unyevu wa nywele.

**Mafuta ya Nazi**

Mafuta ya nazi yana asidi ya mafuta mbayo hupenya shimoni la nywele na kupunguza upotezaji wa protini kutoka kwa nywele.

**Mafuta ya samaki**

Kula mafuta ya omega inayotokana na samaki inasaidia kuboresha nywele kutoka kwenye mizizi, kwa kuwa zimejaa virutubisho na protini.

**Juisi ya vitunguu**

Ikiwa unaweza kumudu harufu ya juisi ya vitunguu, unashauriwa kunywa ili kupata faida zake nyingi.


Kitunguu ni chanzo cha kuaminika cha kukuza nywele na kutibu tatizo la alopecia areata.


**Limao**

Unaweza kutumia maji ya limao au mafuta ya limao, kwani zote zimethibitishwa kuongeza ubora wa nywele na ukuaji wake.

Mafuta ya limao yanaweza kukusaidia kudumisha afya ya ngozi ya kichwa na kuchochea ukuaji wa nywele.







MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Mayai chakula rahisi na kitamu

MAYAI ni chakula chepesi na chanzo kikubwa cha protini.

Unaweza kula chakula hiki muda wowote kwa maana ni rahisi kuandaa na pia kina ladha tamu.

**Mahitaji**

Mayai manne, vitunguu viwili, karoti viwili, pilipili hoho moja, kitunguu saumu, punje mbili, pilipili manga kijiko kimoja kidogo na chumvi.

**Namna ya kuandaa**

Andaa kitunguu maji na kitunguu saumu, menya kisha kata vipande vidogo.

Osha kisha kata pilipili hoho vipande vya wastani. Menya kisha kata karoti kwenye vipande vidogo na hifadhi pembeni.

Pasua yai, weka chumvi kama unavyopenda, koroga vizuri na hifadhi pembeni.

**Namna ya kupika**

Bandika kikaango jikoni acha kipate moto, kisha weka mafuta ya kula. Yakipata moto, weka kitunguu saumu, kitunguu maji.

Koroga vizuri hadi viive. Koroga pamoja, funika acha viive. Baada ya dakika mbili hadi tatu, weka pilipili hoho na karoti kisha koroga pamoja. Acha viive kwa dakika tatu.

Mwagia yai kwenye kikaango, koroga vizuri ili lichanganyike na mboga za majani. Acha iive vizuri upande mmoja, kisha geuza.

Unaweza kuvuruga ili kupata vipande vidogo vidogo au unaweza kuacha kama chapati..

Unaweza kula yai hili kwa chakula chochote kile, ugali, wali au kama kitafunwa chepesi wakati wowote.



## MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Epuka nyumba yako kutitia baada ya muda mfupi kwa kufanya haya

KAMA ilivyo kwa viumbe hai kuathiriwa na mazingira wanayoishi, ndivyo ilivyo pia kwa viumbe visivyo hai ikiwamo nyumba.

Ili kuepuka majengo yasiathirike, ni vyema ubunifu ufanyike katika hali ya ubora wa hali ya juu katika sehemu husika linapojengwa jengo.

Msanifu majengo, Deodatus Charles, anasema hata ujenge nyumba nzuri na kubwa kiasi gani, kama haijabuniwa na kujengwa kwa kuzingatia mazingira ya eneo husika, lazima iwe hatarini kuathirika.

Anasema kabla ya kuanza kujenga nyumba ni lazima ufanye uchunguzi katika eneo husika kubaini endapo kuna magonjwa yanayoweza kuathiri nyumba yako na kufanya ubunifu wa kukabiliana nayo.

Mtaalam huyo anasema endapo nyumba hiyo itajengwa pasipo kufanyiwa ubunifu mzuri, huenda ikaathiriwa na magonjwa hayo.

Anasema miongoni mwa magonjwa yanayoathiri nyumba endapo haijafanyiwa ubunifu mzuri ni kutitia.

Mara nyingi, anasema hutitia kutokana na aina tofauti za udongo, kiwanja au kimo cha msawazo wa msingi kuwa tofauti pamoja na ubunifu hafifu wa udongo kulingana na uzito wa jengo husika.



Ugonjwa mwingine anasema ni nyumba kupitisha maji na kwamba maeneo mengi ya Tanzania yamezungukwa na vyanzo vya maji ambayo yanahitaji usanifu na ubunifu wa hali ya juu wakati wa ujenzi wa nyumba ili kuepuka athari baadae.

"Maeneo mengi ya pwani majengo yake mengi yameathiriwa na tatizo hili na hata limekuwa kero kwa wakazi na watumiaji wa majengo hayo. Baadhi ya majengo yanapitisha maji kwa njia ya sakafu na kuta mithili ya chujio au chemchemu na mara nyingi utagundua kwa kuona ardhi yake inatoa maji wakati wote wa majira ya mwaka.

"Na majengo mengi ya maeneo haya yanaoza na kutitia kwa haraka na hata mashimo ya vyoo vyake huinuka kwenda juu ambalo ni hatari kwa afya za wakazi. Katika hali hii kuta na sakafu huoza kwa haraka kutokana na maji yaliyopo chini ya ardhi kuwa na kemikali mbalimbali zilizopo kwenye maji hayo. Kwa hiyo katika mazingira haya lazima yatumike malighafi sahihi za kuzuia maji hasa wakati wa ujenzi," anasema.

Lingine anasema ni kuoza kwa nyumba na kwamba hali hiyo hutokana na unyevunyevu na kemikali mbalimbali kupitia maji kukaa kwa muda mrefu kwenye kuta na kuathiri ubora wa kuta hizo.

"Na hii husababisha kumea kwa mimea ambayo kusababisha ukungu wa kijani kwenye kuta ambao huzalisha fangasi mbalimbali wanaokula kuta," anasisitiza.

## DONDOO

# Viti vya asili vinanogesha nyumba

**Na Restuta James**

MAPAMBO asilia yanayotokana na miti yaani mbao, fito, magome na makuti vinavyotengenezwa kwa vinaendelea kushika kasi kupamba ndani ya nyumba barani Afrika.

Mtaalamu wa mapambo ya ndani, Jenna Kate, katika chapisho lake la wiki hii anasema aina hiyo ya mapambo haipitwi na wakati akieleza changamoto yake kubwa ni bei kwenye nchi zilizoendelea.

Anataja mapambo hayo kuwa ni viti, meza, stuli na mito; ambavyo vinaweza kutumika ndani ya nyumba na bustanini.

Anasema miongoni mwa samani hizo zipo pia kipande cha gogo kinachoweza kupolishiwa na kubakia na mwonekano wake wa asili kisha kutumiwa kama meza ndogo sebuleni au bustanini.

"Aina hii ya meza ni moja ya bidhaa zinazouzwa sana mtandaoni kutokana na mwonekano wake kuleta uhalisia na uhai ndani ya nyumba," anasema Jenna.

Anafafanua kuwa ziko meza nyingine zinazotengenezwa kwa fito ndogo zikiwa na umbo la ngoma, zinazoongeza mvuto ndani ya nyumba.


Anasema vitu asilia kama mbao na fito vinatumika pia kutengeneza 'holder' ya taa, ambayo itakamilisha seti ya vitu asilia ndani ya nyumba kwa mtu ambaye ameamua kutumia mapambo ya asili.

Kingine ni fremu ya kioo ambayo nayo inaweza kutengenezwa kwa kutumia mbao badala ya aluminiamu au chuma.

"Ukifuatilia masoko makubwa mitandaoni utabaini kwamba hizi ni samani zinazouzwa zaidi japokuwa bei yake kubwa ni changamoto," anasema..



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
SINYWI GONGO KAMA FASHENI, MWENZAKO NAOMBOLEZA!
IMEANDIKWA WAPI?
SIKU NYINGINE TUKITOKA KILABUNI USIKU NITAFUTIE NENO ZURI LA KUMWAMBIA MKE WANGU
'TABATA'
KWA HIYO ULIMWAMBIA VILEVILE KUWA UMESOMBWA NA MAFURIKO WAKATI UJALOWANA?
KWA HIYO BAADA YA KUMFUMANIA UKAAMUA KUM-FUNGISHA NDOA!
HATA WEWE UKIMFUMANIA MKEO FANYA KAMA NILIVYO-FANYA MIMI
SASA MAMLAKA ZIKITOA MATAMKO TUTAZINGATIA
WALISEMA NUNUENI VYAKULA WEKENI NDANI WENGI MKAPUUZA!
WEWE USIJITOE WAKATI SOTE NDIO WALEWALE TUNAOTEMBEA NA MAJIKO MFUKONI, AKILIWI MPAKA TURUDI.
MPE ZA USO HUYO
WAMEBAHATISHA TU, WANASEMA HIVO HIVO ALAFU HAZINYESHI
ILA TUMEJIFUNZA SIKU NYINGINE WAKISEMA ATUBISHI
HUJIELEWI
KINACHOTUPONZA LILE SWALI LETU LA "NYIE MNAJIFANYA MIUNGU WATU?"
KONDA DAI NAULI MBELE DARAJA UTAKUTA LISHASOMBWA HAWATOLIPA!
MKE WANGU KAMA UNABISHA NENDA SHUGHULINI ILA UKIRUDI UTANIKUTA NISHAJINYONGA
BABA YANGU MZAZI ALINITUMA KAMBA ALIJINYONGA NAMWANGALIA HADI KAFA NKAENDA DISKO
AGIZA BIA TUKAZIWAKILISHE KWA WAFIWA
TUTAFUTE NA MADEM WAKUTUFARIJI KABLA HATUJAZIWAKILISHA
MIMI NI 'HENDISAMU' USIJISHAUE
HENDISAMU GANI SURA KAMA UNA-AGWA SURA YA MWISHO!
HAKUNA WAKABAJI?
HUKU UNACHAGUA MWENYEWE AINA YA KABALI
'uswazi'
BAR
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...MAPENZI YA HAWALA UWE NACHO

## HABARI KIMATAIFA

# Marekani yapiga kura ya turufu kutetea Israel kuipiga Gaza

**NEW YORK,** MAREKANI

MAREKANI imetumia kura ya turufu kuzuia azimio lililopendekezwa na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kutaka usitishwaji wa mapigano Ukanda wa Gaza.

Baraza la Usalama lilikutana Ijumaa ya wiki hii kwa ajili ya kujadili azimio la usitishaji mapigano kati ya Israel na Hamas.

Katibu mkuu wa Umoja huo Antonio Guterres alitumia Kifungu cha 99 cha Mkataba wa Umoja wa Mataifa kutaka mapigano hayo yasitishwe.

Azimio hilo lililotayarishwa na Falme za Kiarabu na kuungwa mkono na nchi 100, lilipigiwa kura za ndio 13, kura moja ya hapana iliyopigwa na Marekani, huku Uingereza haikupiga kura.

Wakati jeshi la Israel likiendelea na mashambulizi yake katika miji ya Jabalia na Khan Younis, Baraza hilo la Usalama lilitumia kifungu hicho ambacho kwa miongo kadhaa hakijatumiwa. Kifungu hicho kinamruhusu katibu mkuu kuwasilisha katika baraza la Usalama suala lolote ambalo kwa mtazamo wake linaweza kutishia amani na usalama kimataifa. Hali katika maeneo ya Ukanda wa Gaza imeripotiwa kuwa mbaya kufuatia mashambulio mapya ya vifaru vya Israeli kutoka upande wa kaskazini mwa eneo hilo.

Pia mashambuli makali yanaendelea upande wa Kusini mwa Gaza.

Pamoja na kuwepo kwa shinikizo la usitishwaji wa mapigano jeshi la Israel na wanamgambo wa Hamas wanakabiliana vikali katika viunga vya miji hiyo.

Katika eneo la Kusini hasa katika mji wa Khan Younis, vikosi vya Israel vilifanya mashambulizi ya nyumba kwa nyumba.

Juzi usiku Hamas walitoa video ambayo ilionyesha jinsi operesheni ya Israel ilivyoshindwa kuwakomboa mateka.

Video hiyo ilionyesha picha za mwili wa mtu uliojaa damu na unadhaniwa kuwa wa mateka. Msemaji wa jeshi la Israel (IDF) alisema wanajeshi wawili wamejeruhiwa vibaya wakati wa operesheni inayofanyika ya kuwakomboa mateka sehemu walipohifadhiwa huko Gaza, hata hivyo hakuna aliyepatikana.

**Wakati huo huo,** Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) limesema uwezo wa ugawaji wa mahitaji muhimu Ukanda wa Gaza uko katika hatari ya kuvurugika wakati vita vikiendelea.

Kupitia mtandao wa kijamii wa X, Naibu Mkurugenzi wa BFP, Carl Skau alisema kwamba hakuna chakula cha kutosha na watu wanakufa kwa njaa.

Skau aliandika kwamba maelfu ya watu waliokata tamaa na kuzidiwa na njaa wamejazana katika vituo vya usambazaji wa misaada ya kibinadamu na kambi maalumu.

**RFI**



Zimamoto wakiwajibika katika jengo lililoshambuliwa na majeshi ya Israel katika mji wa Khan Younis kusini mwa Ukanda wa Gaza jana. **PICHA: REUTERS**

# Tshesekedi amchokonoa Rais Paul Kagame

**BUKAVU,** DRC

UHUSIANO kati ya nchi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Rwanda unazidi kuwa mbaya kutokana viongozi wa mataifa hayo kutoleana maneno ya vitisho.

Katika tukio la hivi karibuni, Rais wa DRC, Felix Tshisekedi alimfananisha Rais wa Rwanda, Paul Kagame sawa na aliyekuwa kiongozi wa Nazi Adolf Hitler.

Katika hotuba yake ya kampeni aliyoitoa mjini Bukavu Ijumaa, Tshesekedi alisema akikutana na Kagame atamweleza aache tabia ya Hitler kwa kutaka kujiongezea eneo la nchi yake.

Eneo la mashariki mwa DRC limekumbwa na ghasia kutoka kwa vikundi vya waasi, wakiwamo M23 ambao wanatoka jamii ya Watutsi na kufanikiwa kuteka maeneo mengi tangu kuanza tena mashambulizi 2021.

DRC na mataifa kadhaa ya magharibi ikiwemo Marekani na Ufaransa, yanasema waasi wa M23 wanaungwa mkono na Rwanda.

"Nitazungumza na Rais wa Rwanda Paul Kagame na kumwambia hivi, kwa kuwa alitaka kuwa na tabia kama Adolf Hitler kwa kuwa na malengo ya kujitanua (nchini DRC), ninaahidi ataishia kama Adolf Hitler," Tshisekedi aliuambia umati wa watu waliokuwa wakishangilia.

**BBC**

# Waziri mkuu Burundi afungwa maisha

**BUJUMBURA,** BURUNDI

WAZIRI Mkuu wa zamani wa Burundi, Alain-Guillaume Bunyoni, amehukumiwa kifungo cha maisha jela baada ya kupatikana na hatia ya uhaini ya kutishia kumuua rais na kupindua serikali.

Jenerali Bunyoni, ambaye aliteuliwa nafasi ya Waziri Mkuu Juni 2020, aliachishwa kazi mnamo Septemba 2022, siku chache baada ya Rais Evariste Ndayishimiye kushutumu jaribio la mapinduzi.

Mahakama kuu ya nchi hiyo ilisema waziri mkuu huyo wa zamani anahukumiwa kifungo cha maisha jela kwa makosa saba aliyokuwa akituhumiwa, likiwamo la kupanga njama dhidi ya mkuu wa nchi kupindua utawala wa kikatiba, jaribio la kumuua mkuu wa nchi kwa msaada wa tambiko na kudharau utawala wa kikatiba.

Pia alipatikana na hatia ya kumtukana mkuu wa nchi, waziri mkuu hata kuhatarisha usalama wa ndani wa nchi.

Aidha, alikutwa na hatia ya kujitajirisha kinyume cha sheria na kuyumbisha uchumi.

Mahakama hiyo iliamuru kutaifishwa kwa nyumba zake nne pamoja na kiwanja na magari 14, kwa mujibu wa chanzo hicho.

**RFI**

# Wababe Haiti wawekewa vikwazo

**NEW YORK,** MAREKANI

BARAZA la Usalama la Umoja wa Mataifa limeidhinisha kuwaongeza watu wanne katika orodha ya watu waliowekewa vikwazo wakituhumiwa kuwa viongozi wa vikundi vya kihalifu nchini Haiti.

Hatua hiyo ilifikiwa wakati taifa hilo likikabiliwa na mzozo wa kibinadamu na kuongezeka kwa miito ya kimataifa ya kupeleka wanajeshi wa kulinda amani kuwasaida polisi wa Haiti ambao wameelemewa na vikundi hivyo.

Umoja wa Mataifa umewawekea vikwazo Renel Destina anayeaminiwa kuwa kiongozi mkuu wa kundi la Grand Ravine, Vitel'homme Innocent wa kundi la Kraze Barye, Johnson Andre wa 5 Segond na Wilson Joseph wa kundi la 400 Mawozo.

**DW**

MAKALA

# NI MALEZI AU MAISHA YAMEBADILIKA?



Na Magabilo Masambu

**Najaribu kufikiri, pengine wavumilivu wamekosekana kwenye jamii zetu au kizazi chetu hiki hatuthamini mila na desturi za jamii zetu tena? Kama kuchaguliwa mume au mke lilikuwa jambo baya, kwa nini tunaochaguana leo bado hatuishi pamoja?**

NI ukweli kwamba ndoa za sasa zimekuwa kizungumkuti. Maswali ni mengi kuliko majawabu huku kila mmoja akijiuliza sababu hasa ni nini. Wako wanaosema pengine malezi ya leo si sawa na yale ya zamani. Lakini tunajiuliza hivi wale waliokuwa wakilea zamani siku hizi wameisha? Au pengine changamoto za maisha zimekuwa nyingi?

Wale waliokuwa wakioana bila kufahamiana mbona ndiyo inaonekana walidumu kwenye ndoa zao? Naposema hawakuwa wanafahamiana namaanisha kwamba wake au waume walikuwa wakitafutwa na wazazi husika au ndugu.

Wale wanaofahamiana leo, namaanisha mume na mke, wanakutana kabla ya wazazi kuwafahamu, kisha wanabebana na kupelekana kwa wazazi.

Zamani wazazi ndio walifahamiana kwanza kabla ya wahusika. Lilikuwa jambo la kawaida sana mtoto wa kiume kutoka katika matembezi yake au shuleni anaporejea nyumbani, kukuta ameshaletewa binti wa kuoa!

Leo tunaonana wenyewe na kwamba tumechaguana na tunapendana kwelikweli. Nilichogundua ni kwamba upendo wa leo unafanana na moto wa mabua ya mahindi ambao hulipuka kwa nguvu na kwisha mara moja.

Lakini mapenzi ya zamani najaribu kuyafananisha na moto wa kisiki, ambao unawaka taratibu lakini huku ukichukua muda mrefu kuzimika.

Kuna wakati nimejaribu kufikiri pengine mwingiliano wa mila na desturi umeleta shida.

Hata hivyo, katika kufanya kauchunguzi kangu, nikagundua kwamba hata watu wa jamii moja leo kudumu ni hadithi nzito. Watabebana huko wanazungumza lugha moja, lakini utasikia baada ya siku chache hawako pamoja.

Wako wanaosema hata hizo ndoa tunazosema waliishi sana, waliishi kwa kuvumilia mambo mengi na kwamba kilichokuwa kinawafanya waishi zaidi ni kuheshimu yale makubaliano ya wazee waliowaunganisha.

Inasemekana kwamba walifika mbali zaidi kuonekana kwamba kuachana ilikuwa aibu kwa jamii nzima, hivyo kuwafanya watu waishi pamoja wakiwa hawapendani bali kulinda mila na desturi.

Najaribu kufikiri, pengine wavumilivu wamekosekana kwenye jamii zetu au kizazi chetu hiki hatuthamini mila na desturi za jamii zetu tena? Kama kuchaguliwa mume au mke lilikuwa jambo baya, kwa nini tunaochaguana leo bado hatuishi pamoja?

Wengine wanasema mapenzi leo yamekuwa rahisi sana kiasi cha kufanana na mtu kuingia dukani na kununua Big G, kuitafuna kisha kuitema. Inawezekana ni kweli kwamba kinachopatikana kwa urahisi huwa kinapotea kirahisi pia. Zamani ilikuwa kazi ngumu sana kuanzisha uhusiano. Kwanza namna ya kuwasiliana ilikuwa ngumu. Binti kama hujamvizia kisimani labda mmekutana machungani lakini siku hizi uhusiano asubuhi saa 2:00, saa 4:00 ndoa!

Haimaanishi kwamba wale wote wanaoonana wenyewe wanaachana bado wako wanaodumu, si kweli pia kwamba wale waliokuwa wanatafutiwa walidumu wote lakini tunajaribu kutazama kwa wingi wake inaonekana leo tuaachana sana si ni kweli ndugu zangu? Madhara yake ni kuwa na watoto wengi wa mitaani na kuwabebesha babu na bibi zetu wajukuu ambao hawakustahili kuwalea, maana wao walitulea sisi.

Huu utaratibu wa kutafutiwa pengine ilikuwa njia sahihi zaidi maana maandiko yanasema: "Si vyema huyo mtu awe peke yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye.

Bwana Mungu akafanyiza kutoka katika ardhi kila mnyama wa msituni na kila ndege wa angani akamletea Adamu ili aone atawaitaje kila kiumbe hai jina alilokiita Adamu likawa ndilo jina lake (Mwanaume ndiye anayetakiwa kutoa jina la mtoto lakini siku hizi kuna mambo ya haki sawa haya bana).

"Adamu akawapa majina yao kila mnyama wa kufugwa na ndege wa angani na kila mnyama wa mwituni, lakini hakuonekana wa kumsaidia Adamu aliyefanana naye. Bwana Mungu akamletea Adamu usingizi mzito naye akalala kisha akatwaa ubavu wake mmoja akafunika nyama mahali pake ule ubavu akaufanya mwanamke akamleta kwa Adamu."

Najaribu kutafakari kwa nini Mungu hakuwa ameumba watu wawili baadaye waje wakutane na waoane.

Tunaona hata Adamu aliletewa mwanamke. Hakutafuta mwenyewe ndiyo maana baadhi ya watu wanasema inawezekana mipango ya ndoa tunaikosea kabla ya kuanza. Sababu nyingine zinatajwa ni za kiuchumi. Wako wanaotamani maisha ya haraka haraka wasipoyaona wanakimbia.

Wengine wanadai ahadi nazo zimekuwa chanzo kwamba vijana wanaahidi mambo yasiotekelezeka, kuiga na kujifunza mambo mbalimbali kutoka kwenye ndoa zingine nacho kinatajwa kuwa chanzo, huku wakisema ndoa ni jambo la kipekee halistahili kujifunzwa kutoka kwa mwingine kwa sababu changamoto hazifanani. Watu hawafanani pia kwa hiyo ni vyema kujifunza mengine na kuchukua machache sana mema kwa ajili ya ujenzi wa ndoa yenu kuliko kumeza kila kitu kama dodoki

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**Dar es salaam-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Tumekosa kina Mbaraka Mwinshehe wa kututungia nyimbo za mafuriko*



Na Adam Fungamwango

**Pamoja na kufafanua hivyo, lakini wasanii na wanamuziki ni lazima wajitofautishe kwa kada nyingine, watumie usanii wao kuwasilisha mchango, ujumbe, kuwatia moyo wafiwa kwa njia ya muziki.**

POLENI sana ndugu zetu wa Rufiji kwa maafa mliyoyapata, poleni pia ndugu wote wa Ulanga kwa hasara kubwa zilizotokea. Mafuriko yamekuwa makubwa sana, majumba na mashamba yamefagiliwa, hakikubaki kitu bali vifo na njaa vimewakuta.

"Ndugu eee wa Rufiji na wa Ulanga, kuyanusuru maisha yenu mfanye nini? Myafuate wanayosema viongozi wetu wa taifa."

Huu ni wimbo uitwao 'Poleni Rufiji' ukiwapa pole wakazi wa Rufiji mkoani Pwani na Ulanga kwa mafuriko makubwa zaidi yaliyotokea mwanzoni mwa miaka ya 1970.

Wanamuziki na bendi nyingi ziliingia studio na kutoa nyimbo za kuwapa pole. Mmoja wa wanamuziki hao ni Mbaraka Mwinshehe ambaye alitunga kibao hicho kiitwacho 'Poleni Rufiji.'

Kibao hiki kinaweza pia kikatumika kuwapa pole wakazi wa Katesh, wilaya ya Hanang, mkoani Manyara kwa maafa yanayofanana na hayo yaliyowakumba. Pale kwenye Rufiji na Ulanga, unatoa na kuweka Katesh na Hanang. Ndiyo ni kwa sababu mpaka sasa hakuna msanii au wasanii walitoa nyimbo zinazofanana na hizo.

Mvua kubwa iliyonyesha usiku wa kuamkia Desemba 2, mwaka huu, ilisababisha mafuriko ya tope zito maeneo ya mlimani, lililoshuka chini na kusambaa kwa kasi kubwa kwenye makazi ya watu. Hali hiyo ilisababisha vifo, waathirika na kuharibu nyumba, maeneo ya biashara, magari na miundombinu.

Serikali imeonekana kuwa bega kwa bega na waathirika katika kipindi chote kigumu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, alikatisha ghafla ziara yake Dubai na kurejea haraka nchini kuungana na wananchi wake katika kipindi hiki kigumu, ambapo alielekea eneo la maafa kuwapa pole wafiwa, kuwafariji waathirika na kuwapa moyo kuwa serikali ipo nao bega kwa bega kwa mahitaji yote ya kibinadamu na kijamii hasa kwa kipindi hiki.

Lakini nimeona pia wanasiasa mbalimbali nao wakienda kuwatakia kila la heri na kuwapa pole wafiwa na huu ndiyo utamaduni wa Watanzania enzi na enzi.

Kila kada huwa inatoa mchango kwa namna yake. Wako wananchi watakaojitolea vyakula, damu, nguo na pesa. Hata waandishi wa habari wanajitolea kwa kuandika na kuzipa kipaumbele habari za huko ili kuwafanya wananchi na wasamaria wema kuzidi kuguswa na kuendelea kutoa misaada.

Mpaka sasa naona bado tasnia ya muziki haijafanya kazi yake vizuri. Nilitegemea mpaka sasa baadhi ya wasanii wangekuwa wameshatoa nyimbo kwa ajili ya kuwapa pole waathirika, wakiwapa moyo na kuwaliwaza kwa kilichotokea.

Sana sana, Jumatano iliyopita nimelisikia Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) likitoa wito kwa wasanii kuungana kwa ajili ya kuchangia familia zilizoathirika na mafuriko katika mji wa Katesh. Katibu Mtendaji wa BASATA, Dk. Kedmon Mapana, alisema wako tayari kuwasindikiza wasanii wanaotaka kutoa mchango wao kwa waathirika.

Hilo ni jambo zuri, na inawezekana kuna baadhi ya wasanii wakaenda kutoa misaada, haizuiwi, msaada anatakiwa kutoa mtu yeyote yule.

Pamoja na kufafanua hivyo, lakini wasanii na wanamuziki ni lazima wajitofautishe kwa kada nyingine, watumie usanii wao kuwasilisha mchango, ujumbe, kuwatia moyo wafiwa kwa njia ya muziki.

Hili wala lisingekuwa jambo la ajabu. Wanamuziki wa zamani walifanya sana kazi hii, kwani wao chochote kinachotokea ambacho kinalihusu taifa, hasa jambo zito kama hili, bendi zingekuwa zimeshaingia studio kutoa nyimbo.

Huu ndio mchango mkubwa wa wasanii na wanamuziki kuliko hata misaada mingine.

Hata wakati wa vita vya Nduli Idd Amin mwaka 1978 hadi 1979, wanamuziki hawakupigana vita, lakini nyimbo zao zilikuwa ni silaha tosha kwa adui. Miaka ya 1970, kulitokea mafuriko makubwa Rufiji mkoani Pwani, wanamuziki waliingia studio na kutoa nyimbo za kuwapa pole wafiwa. Labda enzi zile bendi zilikuwa zikirekodi bure kwenye studio za RTD na sasa kurekodi imekuwa gharama. Msanii anatakiwa kutoa pesa zake mfukoni, lakini hadi leo hii studio za Redio ya Taifa zipo.

Nadhani sasa BASATA ingeongea na TBC ili wasanii, na wanamuziki wanaotaka kurekodi nyimbo kwa ajili ya majanga au matukio ya kitaifa iwe bure kwa sababu wanafanya hivyo kwa ajili ya taifa.

Kuna dhana inajengwa kuwa wasanii wa sasa si wabunifu, na uwezo wao ni nyimbo za mapenzi tu, lakini nao wanakataa wakidai hawawezi kutoa pesa zao mfukoni, wale wa zamani walikuwa wanarekodi bure.

BASATA ingeweza kukusanya hata wasanii kina Diamond, Ali Kiba, Harmonize, Mbosso na wengine wengi na kutoa nyimbo mbili au tatu zinazohusiana na maafa hayo, wakaingia studio za TBC wakarekodi zikaingia sokoni na pesa ambazo zingepatikana zingepelekwa kwa waathirika.

Wala haitokuwa ajabu, kwani mwaka 1985, wanamuziki mastaa nchini Marekani wakiongozwa na Michael Jackson na Lionel Richie walifyatua singo iitwayo ,'We Are the World', iliyouza zaidi ya nakala milioni 20 kwa ajili ya kusaidia watoto masikini wa Afrika.

Hivi kizazi hiki tunataka kina Mbaraka wafufuke waje kututungia nyimbo za maafa?

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

SAUDA, binti mmoja mrembo anapata mwanaume na kubahatika kuolewa, lakini anakwenda kuishi kwenye nyumba ya familia ambayo mumewe Kassim na dada yake Havijawa wameirithi kutoka kwa baba yao mzazi. Binti aliona anakwenda kuishi kwa amani ili atengeneze familia yake, lakini kinachomkuta huko anajuta hata kwa nini alikubali kuolewa. Mara nyingi kuolewa ni jambo la kheri, lakini kwa Sauda inakuwa kinyume chake, kwani anakutana na wifi mtata, mkorofi, mmbea, mchonganishi ambaye anaiweka ndoa ya binti huyo aliyeolewa na kaka yake kuwa ya mashaka, tabu, huzuni, isiyokuwa na amani.Hali hii inamchosha Sauda na kulazimika kudai talaka kurudi kwao? Fuatilia kisa na mkasa huu unaosimuliwa kwenye gazeti hili la Nipashe pekee.

# Wifi Kichefuchefu-1

Na Adam Fungamwango
(0716 350534)

HIVI kaka, mhhh, unajua muonekano wako wewe ni tofauti na huyu mwanamke uliyemleta humu ndani!"

"Kwa nini unasema hivyo dada?"

Yaani sijui umetuletea kituko gani, wifi mbaya kama nini, sijui ulivyokuwa unamtongoza ulikuwa umefumba macho, mchoyo mchoyo, hajipendi, mwanamke gani huyu?"

"Dada, mimi sina uhakika sana na unachokisema."

"Wewe kaka umerogwa si bure. Niliambiwa tu, hawa watu kabila lao si la mchezo wana tabia ya kuwawekea limbwata wanaume, nilikuwa siamini, sasa nimemini."

"Sasa nani kawekewa limbwata. Mimi, wewe au wote?"

"Humu ndani mwanaume nani? Nani aliyeoa? Si wewe?"

"Kwa hiyo mimi ndiyo niliyewekewa?"

"Wewe hujioni? Kila ukiambiwa kuhusu mke wako dharau zimekujaa. Hujali, ndiyo kwanza unajibu kwa kejeli kama hivi."

"Kwani dada tatizo hasa ni nini?"

"Hebu kama hivi ukijiangalie yule anaendana na wewe? Hivi ulimuokota wapi?"

"Kwao!"

"Unaona unavyonijibu kwa dharau, nikisema limbwata limekukolea unakataa, tena wewe lile lenyewe kabisa la nyama iliyoungwa na rosti ukapikiwa na wali wa nazi juu."

Yalikuwa ni mazungumzo ya Kassim na dada yake Havijawa. Yalihusiana na mke wa Kassim aliyemuoa miezi mitatu iliyopita.

Ilionekana kabisa kuwa mke wa Kassim na dada yake Havijawa hawaivi.

Kilichomshangaza Kassim ni kwamba hata mwanamke aliyetaka kumuoa mwanzo, pamoja na kwamba walikuwa marafiki na dada yake, lakini mwisho wa siku waligombana.

Siwatu, mwanamke ambaye alikuwa tayari alikuwa ameshamtolea barua kwao. Lakini kulitokea mtafaruku baina yao, wakaachana.

Kassim akaishi kwa miaka minne bila kuwa na mwanamke yeyote mpaka dada yake akamshauri aoe.

Alikuwa anahitaji kuoa, lakini wa kumuoa ndiye hakuwepo. Ugomvi uliotokea baina yake na mchumba wake ambaye alikuwa anaishi naye nyumbani hapo kabla hajamuoa, ulimuathiri sana.

Ulitokana na kumfuma akiwa amesimama na jamaa mmoja wa nyumba jirani maeneo ambayo si mazuri sana na yalimtia wasiwasi.




**Hakutaka ionekane mkewe ana matatizo kwa sababu si kweli, na wale hakutaka kumuudhi dada yake kwa kumwambia ukweli kuwa anachofanya ni uzandiki.**

Si hivyo tu, alishawahi kuambiwa kuwa jamaa huyo anaonekana sana mitaa ya nyumbani kwake na amekuwa akipenda kuongea sana na mwanamke huyo anayeishi naye.

Baada ya kugombana na mchumba wake kuhusu tukio hilo, siku tatu baadaye, Kassim alirejea nyumbani na kukuta nyumba imefungwa.

Alikuwa na funguo ya akiba. Alipofungua ni chumba tu kilikuwa kinamtazama. Cheupeee!

Siwatu alikuwa amekomba kila kitu. Ni siku ambazo dada yake Havijawa alikuwa anaishi Keko kwa bwana yake.

Mwezi mmoja baadaye dada yake naye alikorofishana na bwana'ake, akaamua kukusanya virago vyake na kurejea nyumbani kwao Ubungo Kibangu kwenye nyumba ya baba yake.

Akamkuta kaka yake ambaye naye alikuwa amekimbiwa na mwanamke wake.

Ilikuwa kama mkosi kwa ndugu hao ambao walikuwa wamebaki wawili tu, baada ndugu zao wengine watatu, wanaume wawili na mwanamke mmoja kufariki dunia kwa nyakati tofauti.

Nyumba aliyowaachia baba yake ilikuwa ya vyumba vinne na varanda, kila mmoja akikaa chumba kimoja na viwili wakapangisha.

Waliopangishwa humo walikuwa wanaume tu mabachela, kwani wale wa mwanzo waliokuwa na wake waliondoka kutokana na mdomo wa Havijawa.

Anajulikana Ubungo nzima na hata Keko alikotoka kwa bwana yake kwa tabia ya ukorofi, utata, umbea na uchonganishi.

"Kwanza mwezi wa tatu tangu umuoe mwanamke hata kula ndimu, au udongo hatuoni, kazi michipsi mama, na mikuku, mke gani huyu kaka? Anakula kama mchwa, atakufilisi huyu kama yangu!"

Kwa bahati nzuri Kassim anafahamu tabia ya dada yake, hivyo amekuwa akijibu zaidi kidiplomasia.

Hakutaka ionekane mkewe ana matatizo kwa sababu si kweli, na wale hakutaka kumuudhi dada yake kwa kumwambia ukweli kuwa anachofanya ni uzandiki.

"Nimesikia dada yangu, sasa wewe hasa ulitaka nifanye nini?"

"Kaka hapa namna mke, mpe talaka yake, afadhali umrudie hata Siwatu, au utafute mwingine. Unajua yule Siwatu basi tu ilipitika fitina tu hapa mtaani, ila mimi namuelewa sana!"

Kassim alimtazama dada yake, halafu akakwepesha macho haraka kwa sababu halikuwa jicho la heri na muangaliwaji angebaini tu angejua muangaliaji amekasirika.

"Okay nimekusikia. Tutaangalia itakavyokuwa."

**********************************

Kassim hakupata usingizi. Akawaza maneno ya dada yake kuwa amrudie Siwatu.

"Hivi huyu dada ana wazimu huyu?"

Akamuwaza Siwatu jinsi alivyomfanyia kiasi kwamba ilimuathiri kisaikolojia na kuanza kuchukia wanawake wote.

Hiyo ikamfanya asiwe na mwanamke yeyote kwa miaka mitatu, kabla ya kuanza uhusiano na Sauda kabla ya kumuoa mwaka mmoja tu baadaye.

Kwake Sauda ni zaidi ya mke. Ni mtu aliyemrejesha kwenye ulimwengu wa utu, na ubinadamu.

Kitendo alichofanyiwa na Siwatu kilimfanya kuwa na mawazo, akaangukia kwenye ulevi uliokithiri.

Akikumbuka siku ambayo alimkuta mchumba wake na yule jirani yake, roho kama ilitaka kumpasuka, halafu baadaye kukombewa vitu vyote vya ndani kabla ya kupotelea kusikojulikana, ilimtia simanzi kiasi kwamba ilibadi kidogo apate kichaa.

Kibaya zaidi jamaa yule Kindemba naye alihama maeneo hayo, lakini wiki chache tu baadaye zikaja taarifa kuwa jamaa huyo na Siwatu wako pamoja, wakaishi pika na kupakua maeneo ya Buguruni kwa Malapa.

Hapo alijua kabisa kuwa licha kuishi pamoja, hata samani wanazotumia ni zile ambazo zimechukuliwa na Siwatu ndani kwake.

Kitu hiko kilimfanya si tu kuchanganya, lakini kuwaogopa wanawake na rafiki yake mkubwa alikuwa ni pombe.

Akaapa kutopenda tena maishani mwake. Kama ameumia hivyo moyoni mwake, alihisi kama ikitokea tena mara ya pili akaumizwa, basi anaweza kufa.

Akawa na kazi ya kuulinda moyo wake usijeruhiwa tena kwa mara ya pili kwani sababu inaweza kuwa hatari zaidi kuliko mwanzo.

Siku zote mipango siyo matumizi. Binadamu hupanga, Mungu hupangua. Penzi ni kama ajali, hutokea tu bila kupangwa, kwa yoyote na popote.

Pamoja na kujidhibiti, kutotaka kujiingiza kwenye penzi, na kuwa makini sana, lakini safari hii aliingia kwenye mapenzi kirahisi zaidi kuliko hata mwanzo.

Kwa Siwatu kazi aliifanya. Ilikuwa ngumu mno, lakini kwa Sauda alinaswa kwenye mtego kirahisi sana kiasi kwamba hata yeye mwenyewe kila akikumbuka anabaki anacheka tu.

"Mwanamke huyu!" Anajiambia mwenyewe na kucheka kimoyomoyo kila akikumbuka jinsi alivyokuwa hataki tena wanawake, lakini akaanguka kwenye penzi kiulaini kama kumsukuma mlevi kwenye utelezi.

**INAENDELEA JUMAPILI**

# DULA MAKABILA WEWE NI NOMA!

VIDEO ya ngoma mpya ya Dula Makabila inayoitwa 'Nije Nisije' imemwagiwa sifa baada ya kuleta mapinduzi ya ubunifu katika muziki wa Singeli.

Wimbo huo ambao umetambulishwa siku tatu zilizopita umeonekana kuwavutia wengi kutokana na ubunifu uliofanywa na msanii huyo kwenye video hiyo.

Ndani ya video hiyo ambayo imesheheni waigizaji maarufu nchini, Dulla Makabila ameonekana kama mtoto mchanga aliyekuwa tumboni ambaye anazungumza kuhusu mikasa ya mama yake na kuwauliza wakunga na madaktari kwamba ana uamuzi wake kama aje au asije duniani.





# Joh Makini atoa tiba kwenda nje

RAPA mkali Joh Makini amesema uraia pacha umesaidia wanamuziki wa mataifa mengine ya Afrika kupenya katika nchi za Ulaya na Marekani.

Amesema serikali inatakiwa kufanya jitihada ya kuhakikisha kuwepo na njia ya kurahisisha wasanii kwenda nje ya nchi haraka ili kutatua tatizo hilo.

"Wasanii wa Tanzania wanaweza kwenda nchi mbili bila visa Afrika Kusini na Rwanda, lakini wenzetu hasa Nigeria wana uraia pacha na mataifa mengine hivyo wao ni rahisi kufanya kazi kwa upana zaidi," amesema.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

**SANCHO KUBADILISHWA**
KLABU za Manchester United na Borussia Dortmund zinafanyia kazi mkataba wa kubadilishana ambao utamfanya winga wa England, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 23, kurejea katika klabu hiyo ya Bundesliga - huku mshambuliaji wa Uholanzi, Donyell Malen mwenye umri wa miaka 24 akielekea upande United. (***Sport Bild***)

**CHELSEA YAMKOMALIA OSIMHEN**

CHELSEA ipo tayari kulipa chochote kinachohitajika kumsajili mshambuliaji wa Nigeria, Victor Osimhen mwenye umri wa miaka 24 kutoka Napoli Januari. (***Football Transfers***)

**ERIKSEN KUUZWA**

MANCHESTER United ipo tayari kumuuza kiungo wa kati wa Denmark, Christian Eriksen mwenye umri wa miaka 31 katika dirisha la uhamisho la Januari. (***Football Insider***)

**PALHINHA AWANIWA UNITED**

MANCHSTER United na Liverpool zimejiunga na Klabu zinazomuwania kiungo wa Fulham kutoka Ureno, Joao Palhinha mwenye umri wa miaka 28. (***TeamTalk***)

**BAYERN HAWAWEZI**
BAYERN Munich haina uwezekano wa kumsajili Joao Palhinha mwenye umri wa miaka 28 Januari. (***Sky Sports Germany***)

**RICHARLISON KUUZWA**

KLABU ya Tottenham Hotspur itafikiria kumuuza mshambuliaji wa Brazil, Richarlison mwenye umri wa miaka 26 Januari, huku pia nyota huyo akiwaniwa Saudi Arabia. (***Football Insider)***

**LIVER HAITAFUTI BEKI**

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amepuuza taarifa kwamba klabu hiyo itamtafuta mchezaji mwingine wa kuchukua nafasi ya mlinzi Joel Matip aliyejeruhiwa katika dirisha la usajili la Januari. (***Mirror***)

**LOPETEGUI KUMRITHI COOPER**

KOCHA wa zamani wa Wolves, Julen Lopetegui yuko tayari kuchukua nafasi ya Steve Cooper pale Nottingham Forest baada ya kukataa ofa nono hivi majuzi kutoka kwa Al-Ittihad ya Saudi Arabia. (***Talksport***)

**SANSON ATAKA KUDUMU VILLA**

KIUNGO wa kati wa Aston Villa, Morgan Sanson mwenye umri wa miaka 29 anataka kufanya uhamisho wake wa mkopo kwenda OGC Nice uwe wa kudumu. (***Get France Football News***)

**YORO AGOMBEWA MANCHESTER**

MANCHESTER United iko tayari kushindana na Manchester City kuwania saini ya mlinzi wa Lille, Mfaransa Leny Yoro mwenye umri wa miaka 18. (***Mirror***)

**GREGORIO AGEUKA LULU**
AC Milan na Napoli zinakabiliwa na ushindani kutoka kwa klabu za Ligi Kuu England kuwania saini ya kipa wa Monza, raia wa Italia, Michele di Gregorio mwenye umri wa miaka 26. (***Tuttomercatoweb)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# TEN HAG: MLANGO UPO WAZI SANCHO KUREJEA MAN UTD

**MANCHESTER,** England

●●●Kocha huyo amesema ni juu ya nyota huyo wa England kuamua nini cha kufanya ili....

ERIK ten Hag ameacha mlango wazi kwa Jadon Sancho kurejea kwenye kikosi cha Manchester United, lakini akasema ni "juu yake" mwenyewe.

Sancho hajacheza tangu Agosti baada ya mzozo wa hadharani na Ten Hag na amekuwa akihusishwa kuondoka Old Trafford katika dirisha la usajili la Januari.

Chanzo kimoja kiliiambia ESPN kwamba klabu yake ya zamani ya Borussia Dortmund ina nia ya kumsajili tena mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, pengine katika mkataba ambao unaweza kumfanya mshambuliaji wa Uholanzi, Donyell Malen kuhama kwa njia nyingine, lakini Ten Hag amesema kuna njia ya kurejea hapo United kama akiomba msamaha.

**"Inahusu utamaduni na kila mchezaji lazima alingane na viwango fulani na ilikuwa hivyo," alisema Ten Hag akiwambia waandishi wa habari.**

"Nini kitatokea huko, anajua anachotakiwa kufanya ikiwa anataka kurudi na ni juu yake, anajua anachotakiwa kufanya, ni juu yake mwenyewe.

"Tutaona kitakachotokea. Ni suala la ndani, tutaona kitakachotokea," alisema Ten Hag.

Vyanzo viliiambia ESPN kwamba kuna uwezekano mkubwa kwamba Sancho ataondoka kwenye klabu hiyo Januari kwa sababu mshambuliaji huyo wa England hajaonesha nia ya kuomba msamaha.

Ukiacha kutokuwa na uhakika kuhusu mustakabali wa Sancho, Ten Hag alisema hatarajii dirisha la uhamisho la Januari kuwa na shughuli nyingi kwao.

"Sidhani kama kutakuwa na mengi kwenye dirisha la usajili, lakini tunapaswa kujiandaa ikiwa kuna fursa," aliongeza.

"Ikiwa kuna hali fulani au mshangao, lazima tuwe tayari kuchukua hatua," alisema.

Suala moja lililo mbele ya dirisha hili ni hali ya walinda mlango, ambapo namba moja, André Onana huenda akachaguliwa na Cameroon kwa ajili ya michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika, itakayoanza Januari nchini Ivory Coast Januari.

Kipa Altay Bayindir bado hajacheza mechi yake ya kwanza katika klabu hiyo, na chaguo la tatu Tom Heaton mwenye umri wa miaka 37, hajacheza mechi ya Ligi Kuu kwa takriban miaka mine, lakini Ten Hag alidokeza kuwa hatazami kusajili golikipa mwingine.

"Tunachohitaji ni makipa watatu wazuri sana kwa msimu wa mafanikio na wenye vipaji nyuma, basi hali nzuri ni kipa mmoja au wawili kwa mkopo kwa sababu ni lazima uwaendeleze kila wakati," alisema.

"Tumefurahishwa na kundi tulilonalo sasa, tulikuwa tunaifahamu hali ilivyo na tunatakiwa kulisimamia hilo, kwa hiyo tuna kundi la walinzi imara sana hasa wale watatu wa mwanzo, wote wanaweza kucheza, wote wapo," alisema Ten Hag.

# RONALDO AFIKISHA MICHEZO 1,200



**RIYARH,** Saudi Arabia

CRISTIANO Ronaldo alisherehekea mechi yake ya 1,200 ya kulipwa kwa bao alipoisaidia timu yake ya Al Nassr ya Ligi Kuu ya Saudi Arabia kupata ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya Al Riyadh, Ijumaa.

"Cristiano Ronaldo sasa amecheza mechi 1,200 za kulipwa," taarifa ya Ligi Kuu ya Saudia (Saudi Pro League) ilichapisha kwenye mtandao wa X, huku mchezaji huyo wa zamani wa Real Madrid akikaribia rekodi ya Peter Shilton ambaye anaongoza orodha ya wachezaji wa kiume waliocheza mechi nyingi rasmi.

Ronaldo mwenye umri wa miaka 38 alifunga bao la kuongoza muda mfupi baada ya mapumziko alipounganisha krosi kutoka kwa Sadio Mane, ambaye bao lake lilikakataliwa katika dakika ya kwanza ya mchezo.

Bao hilo lilikuwa la 868 katika maisha ya soka ya Ronaldo.

Mreno huyo aliimarisha hadhi yake ya kuwa mfungaji bora wa ligi hiyo kwa mabao yake 16 katika mechi 16 za msimu huu na kuisaidia timu yake kurejea kwenye ubora wake baada ya kichapo cha mabao 3-0 kutoka kwa viongozi Al Hilal Ijumaa iliyopita.

"Pointi tatu zaidi" aliandika Ronaldo kwenye mitandao ya kijamii.

"Nawashukuru wachezaji wenzangu wote walionisaidia kufikia mechi yangu ya 1,200. Ni safari gani, lakini bado hatujamaliza!"

Al Nassr wanashika nafasi ya pili kwenye msimamo wakiwa na pointi 37, saba nyuma ya Al Hilal, huku Al Riyadh wakishika nafasi ya 14 wakiwa na pointi 16.

Kipa wa zamani wa Englamd, Shilton anakubalika kuwa ndiye anayeshikilia rekodi ya michezo mingi ya kulipwa ya wanaume yenye ushindani mkubwa, ingawa jumla yake ina utofauti.

Baadhi ya tovuti za takwimu zinasema kuwa alicheza jumla ya mechi 1,390 lakini Shilton mwenyewe kwenye mtandano wa X amesema alicheza mechi 1,387.

# Liverpool hawataziba nafasi ya Matip

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp mesema Liverpool hawana uwezekano wa kupata mlinzi mwingine Januari ili kuchukua nafasi ya Joël Matip ambaye amepasuka mishipa yake ya goti katika ushindi wao wa 4-3 dhidi ya Fulham wikendi iliyopita.

Mara nyingi Klopp amekuwa akimpendelea mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 kama mshirika wa Virgil van Dijk katikati mwa safu ya ulinzi ya Liverpool.



Licha ya umuhimu wake katika timu, kocha wa Liverpool alisema haitakuwa rahisi kuchukua nafasi ya Matip katika dirisha la usajili la Januari.

"Katika miaka minane hapa, sielewi hili. Kila mara unazungumza kuhusu uhamisho kana kwamba kitakuwa kitu rahisi zaidi duniani," alisema Klopp akiwaambia waandishi wa habari.

"Leteni tu mchezaji, tafuta fedha yake, kana kwamba tuna fedha zisizoisha, sielewi. Kila mtu, nyinyi mashabiki, kila mtu anazungumza juu yake.

"Yote yanagharimu fedha. Ni lazima awe mchezaji sahihi. Niambie klabu ambayo inataka kuuza kiungo wa kati wa juu ambaye anaweza kuichezea Liverpool?,

"Kwa nini tuanze mchakato huo? Tumejua kwa siku chache tu Joel atakuwa nje kwa muda mrefu, jambo ambalo ni mbaya sana kwetu. Bado tuna sehemu nne za kati ambazo zipo sawa kabisa.

"Haikuwa nchi ya ajabu ambapo unaleta mchezaji wa kati wa kiwango cha kimataifa hadi mwingine awe fiti tena. Klabu nyingine haziweki wachezaji chini ya mti wa Krismasi kwa ajili yetu na kusema: 'mchukue na mtumie kwa muda mrefu kama unahitaji.'

"Sikufikiria juu yake (kununua beki wa kati Januari). Sidhani."

Ibrahima Konaté alianza pamoja na Van Dijk katika ushindi wao wa 2-0 dhidi ya Sheffield United Jumatano, wakati Joe Gomez pia alianza kucheza.

Mkataba wa Matip na Liverpool pia unamalizika mwishoni mwa msimu huu, ikimaanisha kuwa anaweza kuwa ameichezea klabu hiyo mechi yake ya mwisho kwa mujibu wa muda wake wa kupona.

Lakini Klopp alisema kunaweza kuwa na uwezekano wa kuongeza mkataba wa Matip.

"Ningesema hivyo lakini sio uamuzi wangu. Siwezi kusaini karatasi," alisema Klopp.

# Bellingham kutofanyiwa upasuaji wa bega

**MADRID,** Hispania

CARLO Ancelotti amesema hakuna mpango wowote kwa Jude Bellingham kufanyiwa upasuaji wa bega lake lililoteguka, lakini kocha huyo wa Real Madrid hatakataa katika siku zijazo iwapo kiungo huyo ataendelea kusumbuliwa na tatizo hilo.

Bellingham aliteguka bega lake katika mechi ya Madrid ya LaLiga dhidi ya Rayo Vallecano Novemba 5, na kulimfanya kukosa mechi za Braga na Valencia wiki iliyofuata.

Nyota huyo wa England amerejea kwenye timu hiyo, akifunga dhidi ya Cádiz na Napoli, lakini akizungumza katika mkutano na waandishi wa habari jana, Ancelotti alikiri kwamba bado hayuko sawa kabisa.

"Bellingham amekuwa akifanya mazoezi binafsi," alisema Ancelotti.

"Amekuwa akipata ahueni, lazima aangalie bega lake. Anapaswa kufanya kazi maalum ili kuliimarisha, lakini hajapata matatizo yoyote ya kucheza, na kwa maana hiyo, ataimarika kila siku inapopita."

Bellingham amefunga mabao 15 katika mechi 17 akiwa na Madrid tangu ajiunge nayo akitokea Borussia Dortmund majira ya joto yaliyopita, na kiwango chake kilimfanya kutambuliwa wiki hii kwa tuzo ya Golden Boy 2023 ya mchezaji bora wa Ulaya chini ya umri wa miaka 21.

Alipoulizwa tena kuhusu tatizo la bega, Ancelotti alisema kuwa upasuaji kwa sasa sio mojawapo ya njia zinazozingatiwa.

"Sio hivi sasa, hapana," alisema. "Bega ni kiungo maalum. Ikiwa kitateguka tena na tena, unaweza kuhitaji upasuaji. Lakini hivi sasa Bellingham anahisi vizuri."



HABARI MICHEZO

## Gamondi: Tuna kazi kubwa kufuzu

INATOKA UK. 24

kosa yote na kujitoa kwenye michezo iliyobakia," alisema Gamondi.

Alisema kwanza lazima wahakikishe wanapata pointi zote sita kwenye michezo miwili ya nyumbani waliyobakisha kabla ya kupigia mahesabu mchezo wao dhidi ya Al Ahly ambao utakuwa wa mwisho kwenye kundi hilo.

"Tuna michezo miwili nyumbani, tutahakikisha tunapata pointi sita, tunatambua kama wenzetu pia wamejiandaa lakini tutatumia uwanja wa nyumbani kuhakikisha tunapata matokeo ambayo yatatusaidia kufuzu hatua ya robo fainali," alisema Gamondi.

Kocha huyo aliwaomba mashabiki wa timu hiyo kujitokeza kwa wingi katika mchezo wa marudiano dhidi ya Medeama utakaochezwa Desemba 20, Uwanja wa Benjamin Mkapa, kuanzia saa 10.00 jioni.

Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa timu hiyo, Ally Kamwe alisema malengo yao makubwa yalikuwa kutafuta alama tatu lakini wamefanikiwa kupambana na kupata alama moja na sasa wanarejea nyumbani na kusaka ushindi nyumbani dhidi ya Medeama FC.

"Ni kweli tupo kwenye kundi gumu, anayeongoza kundi ana alama tano, akipoteza mechi moja na sisi tukishinda moja basi unaona nafasi ya kupita na kwenda makundi.

"Kama tukishindwa na hatuombei hilo basi tutarudi nyumbani, bado tupo katika uwanja wa vita hatujakata tamaa na kuhakikisha tunapambana kusaka ushindi, tukikosa kuvuka hatua inayofuata basi tutarudi katika malengo yetu mama (ubingwa ligi kuu)," alisema Kamwe.

Kikosi cha Yanga kilitarajiwa kurejea Dar es Salaam usiku wa kuamkia leo, wakitokea Ghana.

## Panga Simba kuwakuta hawa

INATOKA UK. 24

vijana wengi.

Chanzo kinasema kuwa Benchikha anataka kikosi kiwe na wachezaji vijana wengi kwa sababu anapenda falsafa ya mpira wa kasi muda wote wa mchezo.

Kwa upande wa wachezaji wa kigeni, habari za ndani zinasema Willy Onana ni mmoja wa wachezaji anayetarajiwa kuondoka kwenye kikosi hicho ambapo huenda akapelekwa kwa mkopo kwenye klabu ya Rayon Sports ya Rwanda.

Mchezaji mwingine anayetajwa huenda akakutana na panga la Benchika ni Aubin Kramo ambaye bado hajaichezea Simba kwenye michezo ya ushindani kutokana na majeraha na anaweza akarudishwa Asec Mimosas kwa mkopo kwa ajili ya kupata utimamu wa mwili.

# MASHUJAA YAPOKEA FUNGU LA USAJILI DIRISHA DOGO

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI dirisha dogo la usajili likitarajiwa kufunguliwa wiki ijayo, tayari klabu ya Mashujaa FC imepokea fungu la pesa kwa ajili ya kufanya maboresho kwenye kikosi chake.

Mwenyekiti wa Klabu hiyo, Meja Yahaya Mgaya amesema jana jijini Dar es Salaam kuwa tayari ana 'mzigo' kibindoni ambao umetoka juu kwa mabosi wake kwa ajili ya usajili, hivyo kuwataka mashabiki wa soka wa timu hiyo na wakazi wa mkoa wa Kigoma kwa ujumla kutokuwa na wasiwasi.

Mashujaa inamilikiwa na Jeshi la Wananchi (JWTZ), na imecheza Ligi Kuu msimu huu kwa mara ya kwanza.

**Kutokana na hali hiyo, mwenyekiti huyo ametamba kuwa dirisha dogo litakapofunguliwa watafanya usajili wa maana na wana uwezo wa kumsajili mchezaji yeyote wa Kitanzania wanayemhitaji.**

"Sisi tayari tuna fungu la kutosha la kuweza kusajili wachezaji wa aina yoyote hapa Tanzania, lipo tayari na utaratibu umeshafanyika, unajua jinsi ligi ilivyokuwa inakwenda na matokeo ya timu yetu jinsi yalivyokuwa yanatokea, mchakato ulifanyika mapema wapi kwa kuongeza na wapi kwa kurekebisha, kwa hiyo uchambuzi ulishafanyika na tayari fedha za usajili tunazo," alisema Meja Mgaya.

Kwa mujibu wa Bodi ya Ligi, kipindi cha usajili kinatarajiwa kuanza Desemba 16 hadi Januari 15 ambapo timu mbalimbali za Ligi Kuu, Championship, 'first league' na Ligi ya Wanawake zitakuwa kwenye pilikapilika za kusaka wachezaji ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kuongezea nguvu vikosi vyao.

Mashujaa ilianza kwa kishindo ligi msimu huu, lakini baadaye hali ikageuka na mpaka sasa haijashinda mechi yoyote ya ligi tangu Septemba 16, ilipoichapa Ihefu FC mabao 2-0.

Imecheza mechi saba mfululizo bila kupata ushindi, ikitoa sare mbili na kupoteza mechi tano na kwa sasa inashika nafasi ya 15 kwenye msimamo wa ligi ikiwa na pointi tisa kati ya mechi 10 iliyocheza.



Wachezaji wa timu ya mpira ya Kikapu ya TMK, Dodi Kaisi (kulia), na Norbert Mwakajila, wakiwania mpira wakati walipokuwa wakifanya mazoezi katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mbuni FC yaiengua Biashara nafasi ya pili Championship

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Mbuni FC imepanda hadi nafasi ya pili ya Ligi ya 'Championship', baada ya kuifunga Copco FC mabao 2-1 katika mechi ya raundi ya 14 iliyochezwa juzi, Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza.

Matokeo hayo yanaifanya Mbuni FC kukaa kwenye nafasi ya pili, ikiiengua Biashara United iliyokaa kwa muda baada ya kuisulubu Cosmopolitan mabao 2-0 katikati ya wiki hii.

Mbuni FC imefikisha pointi 27 sawa na Biashara United, lakini zimepishana idadi moja tu ya bao la kufunga.

Mbuni FC ina mabao 23, wakati Biashara United inayoshika nafasi ya tatu sasa, ina mabao 22, huku Pamba FC nayo ikiwa na pointi 27, lakini imefunga mabao 19 tu, yenyewe inashika nafasi ya nne.

Ligi hiyo inaongozwa na Ken-Gold yenye maskani yake jijini Mbeya, ambayo mpaka sasa ina pointi 29.

Mabao ya Mbuni FC yalifungwa na Baraka Mwangosi, huku straika wa zamani wa Mwadui wakati huo ikiwa Ligi Kuu, Salim Aiyee akipachika bao la pili kwenye mchezo huo, likiwa ni bao la tisa kwenye ligi na kuwa mmoja wa vinara wa ufungaji kwenye ligi hiyo mpaka sasa.

Wakati timu tatu zikiwa zimefungana pointi 27, timu mbili, Mbeya Kwanza na TMA nazo zina pointi 26 kila mmoja, lakini Mbeya Kwanza ikiwa juu kwa idadi kubwa ya mabao, ikipachika mabao 20, TMA ikiwa nayo 10 tu.

Timu mbili za juu zitapanda daraja moja kwa moja na kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2024/25, huku moja itakayoshika nafasi ya tatu itacheza mechi za mchujo kabla ya kupanda kama ikifanya vizuri kwenye michezo yake hiyo.

# Michezo

Jumapili Desemba 10, 2023

Nipashe




UKURASA 22

**Ronaldo afikisha michezo 1,200**

# Gamondi: Tuna kazi kubwa kufuzu robo fainali

## ●●● Amesema watalazimika kusaka ushindi katika michezo yote kitu ambacho...

**Na Saada Akida**

BAADA ya kushuhudia timu yake ikipata sare ya pili mfululizo kwenye michezo yake ya Kundi D ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha wa Yanga, Miguel Gamondi amekiri kuwa kwa sasa wana kazi kubwa na ngumu ya kufanya kuweza kufuzu hatua ya robo fainali ya michuano hiyo.

Gamondi amesema pamoja na kuwa michezo yote iliyobaki ni migumu, wanatakiwa kupambana kuhakikisha wanavuna alama tatu kama kweli wanataka kuvuka hatua ya makundi na kutinga robo fainali.

Juzi Yanga ilitoka sare ya bao 1-1 wakiwa ugenini dhidi ya Medeama FC matokeo yaliyowafanya kuendelea kuburuza mkia kwenye kundi lao wakiwa na pointi mbili kutokana na michezo mitatu waliyocheza wakizidiwa kwa pointi tatu na vinara, Al Ahly huku CR Belouizdad na Medeama zenyewe zikifikisha pointi nne kila mmoja.

Yanga imebakisha michezo mitatu kumaliza hatua ya makundi ya michuano hiyo, ambapo michezo miwili itachezwa nyumbani dhidi ya Medema na CR Belouizdad na mwingine watacheza ugenini mbele ya Al Ahly nchini Misri.

**Baada ya kuisha mchezo wa juzi, Gamondi alisema mechi hiyo ilikuwa ya ushindani mkubwa na kuwasifu wapinzani wao kuwa walicheza vizuri na wao (Yanga) wanapaswa kujilaumu kwa nafasi walizopoteza.**

“Bado tuna kazi kubwa ya kufanya.., kundi letu limekuwa kundi gumu kutokana na aina ya matokeo yaliyopatikana, tunapaswa kupambana na kufanya kazi kubwa kwenye michezo iliyobaki kuweza kufuzu,” alisema Gamondi.

Alisema mchezo wa juzi dhidi ya Medeama FC wachezaji wake walipambana mpaka filimbi ya mwisho lakini walikosa umakini na bado kuna kazi ya kufanya ili kuondoa makosa aliyoyaona.

“Hatua hii ya makundi ni ngumu sana, kila timu inapambana kuhakikisha inapata matokeo mazuri katika mechi zake, naamini bado tuna nafasi ya kucheza hatua inayofuata kama tutarekebisha ma-

INAENDELEA UK. 23



Winga wa Yanga, Max Nzengeli akipambana na mabeki wa Medeama FC wakati wa mchezo wao hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika juzi kwenye uwanja wa Baba Yaro nchini Ghana, timu hizo zilifungana bao 1-1. **PICHA: MTANDAO**

# Panga Simba kuwakuta wachezaji hawa



**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imeanza mchakato wa kuachana na baadhi ya wachezaji wake wakongwe na mastaa wa ndani na nje kwa ajili ya kuanza kukisuka upya kikosi hicho.

Taarifa kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema kuwa inakusudia kuwatema wachezaji mastaa watano kipindi cha dirisha dogo la usajili linalotarajiwa kufunguliwa Desemba 16 na kumalizika Januari 15, huku zoezi hilo likitarajiwa kuendelea mwishoni mwa msimu huu.

Simba ambayo kwa sasa inafundishwa na Mualgeria, Abdelhak Benchikha inataka kutengeneza kikosi kingine kipya kitakachochukua nafasi ya hiki ambacho wengi wanaona kimeshuka kiwango baada ya wachezaji wake kukaa kwa muda mrefu ambapo baadhi yao wakiwa kikosini humo tangu mwaka 2013.

Chanzo kinasema tayari mkataba wa Simba na nahodha wake John Bocco unatamatika kipindi cha dirisha dogo na tayari wanajiandaa kuachana naye.

“Benchikha, ambaye amechukua nafasi ya Roberto Oliveira, anataka kusajili wachezaji wake ambao anaona watamfaa na sisi tumempa mamlaka ya kumuondoa mchezaji yeyote na kumleta anayemtaka, kwa kuanzia anataka wachezaji watano waachwe ndani ya dirisha dogo ili apate nafasi ya kusajili wachezaji wengine,” alisema mmoja wa viongozi wa klabu hiyo ambaye hakutaka jina lake liwekwe wazi.

Inasemekana mchezaji wa kwanza ambaye ameshapewa mkataba wa kuitumikia klabu hiyo mpaka sasa ni mshambuliaji kutoka Mtibwa Sugar, Ladack Chasambi ambaye amepandishwa msimu huu na klabu hiyo kutoka kikosi cha vijana chini ya miaka 20.

Chasambi, ambaye alikuwa gumzo kwenye ligi ya vijana msimu uliopita na sasa anafanya vyema kwenye Ligi Kuu, anadaiwa kuwa mmoja wa wachezaji watakaokisuka kikosi kipya cha Simba kinachotarajiwa kuwa na

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >